JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE) 2025

## KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE) 2025

# 121 KISWAHILI

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2025**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ..................... IV

1.0 UTANGULIZI ..................... 1

2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI ..................... 3

2.1 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA ..................... 3
2.1.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ..................... 3
2.1.1.1 Swali la 1: Ufahamu ..................... 3
2.1.1.2 Swali la 2: Matumizi ya Sarufi ..................... 10
2.1.1.3 Swali la 3: Matumizi ya Sarufi ..................... 15
2.1.1.4 Swali la 4: Utumizi wa Lugha ..................... 20
2.1.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAREFU ..................... 27
2.1.2.1 Swali la 5: Utungaji ..................... 27
2.1.2.2 Swali la 6: Maendeleo ya Kiswahili ..................... 33
2.1.2.3 Swali la 7: Maendeleo ya Kiswahili ..................... 40
2.1.2.4 Swali la 8: Utumizi wa Lugha ..................... 47
2.2 SEHEMU YA II: KISWAHILI KARATASI YA PILI ..................... 57
2.2.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ..................... 57
2.2.1.1 Swali la 1: Maendeleo ya Fasihi Simulizi ..................... 57
2.2.1.2 Swali la 2: Fasihi kwa Ujumla ..................... 61
2.2.1.3 Swali la 3: Maendeleo ya Fasihi Simulizi ..................... 65
2.2.1.4 Swali la 4: Usanifu wa Maandishi ..................... 71
2.2.2 SEHEMU B MASWALI YA MAJIBU MAREFU ..................... 77
2.2.2.1 Swali la 5: Uhakiki wa Ushairi ..................... 77
2.2.2.2 Swali la 6: Uhakiki wa Ushairi ..................... 84
2.2.2.3 Swali la 7: Uhakiki wa Riwaya ..................... 91
2.2.2.4 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya ..................... 98

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA ..... 107

4.0 HITIMISHO ..................... 108

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ..................... 108

Kiambatisho A : UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MWAKA 2025 ..................... 110

Kiambatisho B : ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MWAKA 2024 NA 2025 ..................... 111

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita mwaka 2025 ili kutoa mrejesho wa matokeo ya mtihani huo kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakuza mitaala na wadau mbalimbali wa elimu ili kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika somo la Kiswahili kwa mtihani ujao.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho inayolenga kuonesha mafanikio ya mfumo wa elimu katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa watahiniwa wa Kidato cha Sita. Kimsingi, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani huu unalenga kuonesha dhahiri maarifa ambayo mfumo wa elimu uliweza au haukuweza kuwapa watahiniwa katika somo la Kiswahili kwa kiwango cha Sekondari, Kidato cha Tano hadi cha Sita.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuonesha sababu za watahiniwa kufanya vizuri, vibaya, au kwa kiwango cha wastani katika maswali/mada mbalimbali zilizopimwa. Ripoti hii inaonesha baadhi ya sababu zilizowafanya watahiniwa kufanya vizuri mtihani huu kama vile kuwa na uelewa mzuri wa mada na uzingatiaji mkubwa wa matakwa ya swali. Pia, sababu za watahiniwa kuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu zimeelezwa kuwa ni pamoja na kutoa majibu yasiyojitosheleza. Aidha, sababu zilizofanya watahiniwa wachache kupata alama hafifu katika majibu yao zimefafanuliwa kama vile kutoelewa matakwa ya swali, uwezo mdogo wa kuelezea dhana mbalimbali kwa ufasaha, udhaifu katika kutathmini maandishi ya kisanaa, na kutokuelewa dhana mahsusi zinazohusiana na somo la Kiswahili kwa ujumla.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa, mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau wote wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ili kuondoa changamoto chache zilizobainishwa katika taarifa hii. Vilevile, Baraza linaamini kuwa kiwango cha ufaulu katika somo hili kitaendelea kuwa bora zaidi iwapo mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa hii yatazingatiwa ipasavyo.

Mwisho, Baraza linatoa shukurani za dhati kwa wote walioshiriki katika mchakato wa uandishi wa taarifa hii.



Prof. Said Ally Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua ufaulu wa watahiniwa katika Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita uliofanyika mwezi Mei mwaka 2025. Mtihani huu uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Kiswahili kwa Kidato cha Tano na Sita. Mtihani ulikuwa na karatasi mbili ambazo ni 121/1 Kiswahili 1 na 121/2 Kiswahili 2. Mtihani 121/1 Kiswahili 1 ulitahini mada za *Ufahamu na Ufupisho*, *Matumizi ya Sarufi*, *Tafsiri na Ukalimani*, *Utungaji*, *Maendeleo ya Kiswahili* na *Utumizi wa Lugha*. Mtihani wa 121/2 Kiswahili 2 ulitahini mada za *Maendeleo ya Fasihi Simulizi*, *Fasihi kwa Ujumla*, *Usanifu wa Maandishi*, na *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*.

Mtihani wa 121/1 Kiswahili 1 ulikuwa na sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali manne (4) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu B ilikuwa na maswali manne (4) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu (3). Swali la tano (5) lilikuwa la lazima.

Mtihani wa 121/2 Kiswahili 2 ulikuwa na sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali manne (4) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu B ilikuwa na maswali manne (4) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu (3). Swali la tano (5) lilikuwa la lazima.


Jumla ya watahiniwa 40,689 walifanya mtihani wa Kiswahili. Miongoni mwao, wavulana walikuwa 18,814 na wasichana walikuwa 21,875. Takwimu zinaonesha kuwa somo hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa watahiniwa 40,537 sawa na asilimia 99.98 walifaulu kwa kupata daraja A hadi S na watahiniwa nane (8) pekee ndio waliofeli na kupata daraja F. Jedwali Na. 1 linaonesha ufaulu wa watahiniwa kimadaraja kwa mwaka 2025.

**Jedwali Na.1: Ufaulu wa Watahiniwa Kidaraja Mwaka 2025**

| **Jinsi** | **Waliofanya** | Ufaulu (%) | **Gredi za Ufaulu** (%) | | | | | | **Waliofeli** (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **A** | **B** | **C** | **D** | **E** | **S** | **F** |
| Wavulana | 18,814 | 99.98 | 0.44 | 22.61 | 53.85 | 20.20 | 2.24 | 0.07 | 0.02 |
| Wasichana | 21,875 | 99.98 | 0.67 | 26.94 | 54.85 | 16.15 | 1.18 | 0.04 | 0.02 |
| Jumla | **40,689** | **99.98** | **0.56** | **24.94** | **54.39** | **18.02** | **1.67** | **0.05** | **0.02** |

Jedwali Na. 1 linaonesha takwimu za ufaulu wa watahiniwa kimadaraja katika somo la Kiswahili kwa mwaka 2025. Kwa ujumla, ufaulu wa Daraja A hadi S kwa wavulana na wasichana unalingana kwani asilimia 99.98 walifaulu. Aidha, watahiniwa waliokuwa na

Daraja F ni asilimia 0.02. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wasichana walikuwa na ufaulu mzuri katika madaraja ya juu A, B na C. Hata hivyo, ufaulu wa wasichana katika madaraja ya chini D, E na S ulipungua, jambo linalodhihirisha kuwa, ufaulu wa wasichana ulikuwa wa juu zaidi kuliko ufaulu wa wavulana. Chati Na. 1 inaonesha ulinganifu wa ufaulu wa watahiniwa kwa kila daraja kwa mwaka 2023, 2024 na 2025.




**Chati Na. 1:** Ulinganifu wa *Ufaulu wa Watahiniwa Kimadaraja*

Katika Chati Na. 1, takwimu zinaonesha kuwa asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika madaraja kwa mwaka 2025 ulipungua katika Daraja A na B. Aidha, ufaulu uliongezeka katika Daraja C, D, E, S na F kwa mwaka 2025, hali inayoashiria kushuka kwa ufaulu katika somo hili kwa asilimia 0.02. Hata hivyo, takwimu za matokeo ya somo hili katika miaka mitatu (2023 – 2025) zinaonesha kuwa ufaulu ni mzuri kwani watahiniwa wengi walifaulu katika madaraja ya juu (B na C) na ufaulu katika madaraja ya chini ulikuwa na watahiniwa wachache.

Viwango vya ufaulu wa madaraja vilikuwa A (80-100) bora sana, B (70-79) vizuri sana, C (60-69) vizuri, D (50-59) wastani, E (40-49) inaridhisha, S (35-39) hafifu, na F (0-34) feli. Uchambuzi zaidi umefanyika ili kubainisha jinsi maswali yalivyojibiwa, namna yalivyopaswa kujibiwa na changamoto zilizojitokeza katika kujibu maswali mbalimbali. Uchambuzi umezingatia matokeo ya watahiniwa yaliyowekwa katika viwango vitatu vya ufaulu yaani vizuri, wastani, na hafifu. Kiwango kizuri cha ufaulu ni alama 60 hadi 100, wastani ni alama 35 hadi 59, na ufaulu hafifu ni alama 0 hadi 34. Aidha, chati na majedwali yametumika kufafanua viwango vya ufaulu, ambapo katika kila chati au jedwali, rangi nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu, rangi ya njano ufaulu wa wastani,

na rangi ya kijani ni ufaulu mzuri. Vilevile, sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatanishwa katika kila swali ili kudhihirisha maelezo ya uchambuzi huu.

## 2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI

Uchambuzi wa majibu kwa kila swali umefanyika ili kuonesha ufafanuzi wa kina wa majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kila swali na kuonesha maswali yaliyojibika kwa kiwango kizuri, cha wastani, na kiwango hafifu. Vilevile, sababu za ufaulu wa watahiniwa zimeelezwa bayana kwa kila swali.

### 2.1 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA

Karatasi ya kwanza imegawanyika katika sehemu A na B. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ni kama unavyoonekana katika sehemu zifuatazo:

#### 2.1.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na alama kumi (10).

##### 2.1.1.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali lilitoka katika mada ya *Ufahamu na Ufupisho*. Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa wa kusoma shairi kisha kujibu maswali yatokanayo na shairi hilo. Swali lilikuwa na vipengele vitano ambavyo ni (a) hadi (e).

Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kuandika kichwa cha shairi kinachofaa kisichozidi maneno mawili. Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi maana ya misemo aliyopewa kama ilivyotumika katika shairi alilosoma. Kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa kueleza namna mwandishi anavyowataka wanadamu wawe katika ubeti wa tatu. Kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi mawazo makuu manne ya mshairi, na kipengele (e) kilimtaka mtahiniwa kuelezea jambo linalozungumziwa na mshairi katika ubeti wa mwisho. Shairi hilo ni hili lifuatalo:

*Maisha ni safari ya chombo,*
*Na dunia ni bahari,*
*Shughulika na sukani,*
*Mwanadamu acha kucheza na bahari.*

*Sisiti kusema tahadhari,*
*Mwanadamu twaa ngao,*
*Dunia humlemea mfitini,*


*Humsimanga mwenye choyo.*

*Vizuri kujiokoa, ubora kuokoana,*
*Kati ya maisha yetu,*
*Tusisahau wosia kupendana,*
*Tusitweze kiumbe wala mtu.*

*Usipaparike dunia ikikusibu,*
*Tafakari kwa kina, kabla hujaamua,*
*Dunia busara haitaki nguvu,*
*Maisha hayamchukizi ayachukuaye kwa heshima.*

*Si hekima kusema yote makosa,*
*Kila cheusi kina cheupe,*
*Si busara yote kuyapurukusha,*
*Katika uamuzi yafaa kuwa mpole.*

Swali lilijibiwa na watahiniwa 40,688 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri sana kwa kuwa watahiniwa 40,001 sawa na asilimia 98.31 walifaulu kwa kiwango kizuri hadi cha wastani. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 2**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Katika Chati Na. 2, watahiniwa 35,331 sawa na asilimia 86.83 walikuwa na ufaulu wa juu kuanzia alama 6 hadi 10, watahiniwa 4,670 sawa na asilimia 11.48 walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5, na watahiniwa 687 sawa na asilimia 1.69 walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa wengi (86.83%) walikuwa na ufaulu wa juu wa alama 6 hadi 10. Watahiniwa hao walionesha kuwa na uelewa wa kutosha wa kifungu cha ushairi kutokana na kuwa na umahiri kuhusu mada ndogo ya *Ufahamu wa Kusoma*. Aidha, watahiniwa waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vingi vya swali hili na kukidhi matakwa ya swali ipasavyo. Vilevile, waliweza kuandika kichwa sahihi cha shairi kwa herufi kubwa kama vile; MAISHA DUNIANI/MAISHA NI SAFARI/MAISHA BAHARI na DUNIA NI BAHARI katika kipengele (a). Katika kipengele (b) walieleza kwa ufupi maana ya misemo waliyopewa kama ilivyotumika katika shairi ambapo (i) Mwanadamu twaa ngao; ulimaanisha *mwanadamu kuchukua tahadhari na kutenda lilo jema*, (ii) Dunia ni Bahari kuwa; ulimaanisha *dunia ina mambo mengi/dunia ni pana/dunia ni kubwa*, (iii) Kila cheusi kina cheupe; ulimaanisha kuwa *mwanadamu ana mabaya na mema na asichukuliwe kwa upande mmoja tu*.

Vilevile, katika kipengele (c) walieleza kwa usahihi namna ambavyo katika ubeti wa tatu mwandishi anawataka wanadamu wawe; yaani *kupendana na kuthaminiana.* Kipengele (d) walieleza kwa ufupi mawazo makuu manne ya mshairi kuwa: (i) *kujihadhari kwani maisha yanabadilika*, (ii) *Kila mtu ana mazuri na mabaya yake*, (iii) *tusidharau wengine bali tupendane* na (iv) *umuhimu wa kujilinda dhidi ya uovu*. Pia, katika kipengele (e) walieleza kwa usahihi jambo linalozungumziwa na mshairi katika ubeti wa mwisho kuwa ni vyema *kuwa na sitara kwa wengine kwani kila mtu anayo mema na mabaya, hivyo inabidi kufanya maamuzi kwa tahadhari*. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

1. (a) Kichwa cha shairi ni MAISHA DUNIANI

(b) (i) Mwanadamu twaa ngao
Msemo huu una maana ya kuchukua tahadhari juu mambo mbalimbali katika maisha ambayo yanaweza kukuletea madhara na matatizo katika maisha yako mfano uchoyo, ugomvi, wizi na mengine yafananayo na hayo.

(ii) Dunia ni bahari
Msemo huu una maana ya kitasuria kwamba dunia ni kubwa na ina mambo mengi mazuri na mabaya. Mwandishi anamtaka mwanadamu kuwa makini na bahari (Dunia) kwa kuepuka mambo maovu katika jamii kwani yana madhara kwa mtu binafsi na taifa kwa ujumla.

(iii) Kila chausi kina cheupe.
Msemo huu una maana ya kwamba kila mtu anayeonekana ni mbaya au mtenda maovu kuna mambo mengine anayoyatenda ambayo ni mema pia. Mfano mtu anaweza kuwa mwenye maneno makali lakini mtu huyohuyo akasaidia watu mbalimbali wasiojiweza katika jamii.

(c) Katika ubeti ~~watatu~~ wa tatu mwandishi ana watak wanadamu kujiweka wenyewe kwa kuepuka mabaya na kufanya mambo mema. Pia anawataka wanadamu kupokea ushauri mzuri pale unapoona mwanadamu mwenzako anaenda tofauti ni muhimu kumshauri; rejea ushairi wa tatu mwandishi anaposema
"Vizuri kujiokoa, ubora kuokoana,

4. Kati ya maisha yetu,
Tusisahau wosia kupendana,
Tusitweze kiumbe wala mtu."

(d) Mawazo makuu ya mshairi ni kama yafuatayo

(i) Umakini katika kufanya maamuzi.

Mshairi anaitaka jamii kuwa makini katika kufanya maamuzi pasipo kukurupuka. Mfano katika ubeti wa nne Mwandishi anathibitisha hilo anaposema!

"Usipaparike dunia ikikusibu,
Tafakari kwa kina, kabla hujaamua
Dunia busara haitaki nguvu,
Maisha hayamchukizi ayachukuaye.

(ii) Upendo miongoni mwa wanadamu.


Katika shairi hili Mwandishi anawataka wanadamu kuwa na upendo kwa kusaidiana, kupendana na kupeana ushauri na wosia. Mfano katika ubeti wa tatu Mwandishi anathibitisha haya anaposema!

" Vitani kujitoa, Ubora kushikana,
Kati ya maisha yetu
Tusisahau wosia kupendana,
Tusitweze kiumbe wala mtu.

(iii) Kuwa na tahadhari/ Kuchukua tahadhari katika dunia.

Tahadhari hii ni ile ya mambo mabaya kunai yana weza kuleta madhara katika maisha ya mtu. Kwa mfano katika ubeti wa pili Mwandishi anasema!

"Usiti kusoma tahadhari,
Mwadamu twaa ngao,
Dunia humlemea mfitini,


1. Humsimange Mwenye choyo."

(iv) Maisha ni Safari ndefu.

Dhamira hii inajitokeza ktk ~~Saf~~ Shairi hili ikiwa na maana kuwa Mwadamu anaweza kadhaa ya kuishi duniani. Katika maisha hayo inem pasa kutenda mema ili kuishi vizuri mfano katika ubeti wa kwanza Mwandishi anasema!

"Maisha ni Safari ya chombo,
na Dunia ni bahari,
Shughulika na Sukani;
Mwanadamu acha kuchoza na bahari."

Katika ubeti wa Mwisho Mwandishi anazungumzia kuwa hakuna Sababu ya kumuongelea Sana mtu mbaya kwani nayo yapo mazuri aliyonayo. Pia Mwandishi anazungumzia kuwa katika kufanya Maamuzi, utulivu unahitajika ili kufanya maamuzi Sahihi na bora. Rejea ubeti wa mwisho mwandishi anaposema!

"Si hekima kulema yote makosa,
Kila chonda kina cheupe,
Si busara yote kuyapurukusha,
Katika Yamuzi Yafaa kuwa mpole".

**Kielelezo Na. 1.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 1


Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi vipengele vyote vitano na kupata alama za juu.

Aidha, asilimia 11.48 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 3.3 hadi 5.5 kutokana na kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa vingine. Baadhi yao, walieleza maana za misemo kati ya mmoja hadi miwili badala ya misemo mitatu waliyopewa katika kipengele (b). Vilevile, walieleza kwa usahihi mawazo makuu kwa kutoa hoja moja hadi mbili badala ya nne kama ilivyotakiwa katika kipengele (d). Hata hivyo, watahiniwa wengi katika kundi hili waliweza kujibu kwa usahihi kipengele (a) kwa kuandika kichwa sahihi cha shairi na kwa herufi kubwa. Pia, walieleza kwa usahihi namna mwandishi anavyowataka wanadamu kuwa yaani *kupendana na kuthaminiana* katika kipengele (c). Vivyo hivyo, walieleza kwa usahihi jambo analozungumzia mwandishi

katika ubeti wa mwisho kuwa, *kila chenye ubaya huwa na jema pia* katika ubeti wa mwisho katika kipengele (e), hivyo kupata alama za wastani.

Licha ya ufaulu mzuri wa swali hili, watahiniwa wachache sawa na asilimia 1.69 walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3. Watahiniwa hao walionesha kukosa uelewa wa kifungu cha ushairi walichopewa. Baadhi yao walijibu kwa usahihi kipengele kimoja au viwili kati ya vipengele vitano walivyopewa. Aidha, kati yao watahiniwa 73 walishindwa kujibu kipengele hata kimoja, hivyo kupata 0. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kipengele (b) alieleza maana ya misemo isivyo sahihi kama vile (i) Mwanadamu twaa ngao kuwa ni *wanadamu kushikamana na kushirikiana*, (ii) Dunia ni Bahari kuwa ni *elimu haina mwisho* na (iii) Kila cheusi kina cheupe kuwa *sio kila mtu akufanyiaye mabaya nawe umtendee mabaya*; maana ambazo hazihusiani na shairi alilopewa.

Mtahiniwa mwingine katika kujibu kipengele (c), aliandika *mwandishi anataka watu wasiwe na tabia mbaya* badala ya kupendana na kuthaminiana kwa watu ambalo ndilo jambo alilozungumzia mwandishi katika shairi lake. Pia, alitaja mawazo makuu ya mshairi yasiyo sahihi katika kipengele (d) kama vile (i) *Elimu*, (ii) *Maisha bora*, (iii) *ubinafsi* badala ya wazo kuu la kujihadhari kwa kuwa maisha yetu yanabadilika, kutumia busara kutatua tofauti zetu, kuheshimiana kwa kuwa kila mtu ana mazuri na mabaya, kupendana, kuthaminiana na kujilinda dhidi ya uchoyo. Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya mtahiniwa aliyejibu vibaya kwa kushindwa kukidhi matakwa ya swali hili.


1 (a) Kichwa cha habari ni Maisha.
(b) (i) Mwanadamu chuka Ngao
(ii)
(iii) Ni busara yote kusapuru kusha
(c) Anataka kujuokoa ubora kuokoana kati ya Maisha yetu
(d) Mawazo makuu ya Mwandishi ni pamoja na
(e) Katika uamuzi ya faa kuwa mpole.


**Kielelezo Na. 1.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 1

Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili. Katika kipengele hiki mtahiniwa, (a) aliandika kichwa cha shairi kwa neno moja badala ya mawili kama swali lilivyomtaka. Pia, katika kipengele (b) hadi (e) alitoa majibu yasiyo sahihi hivyo, kupata alama 1.

### 2.1.1.2 Swali la 2: Matumizi ya Sarufi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Sarufi* hususani mada ndogo ya *Ngeli za Nomino*. Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu ngeli za nomino. Swali lilimtaka mtahiniwa kuonesha ubora na udhaifu wa kuainisha ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimamboleo.

Swali lilijibiwa na watahiniwa 40,688 sawa na asilimia 100. Swali hili lilijibiwa kwa wastani ambapo watahiniwa 20,991 sawa na asilimia 51.59 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3.5 hadi 10. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 3**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*

Katika Chati Na. 3, watahiniwa 12,792 sawa na asilimia 31.44 walikuwa na ufaulu wa juu kuanzia alama 6 hadi 10, watahiniwa 8,199 sawa na asilimia 20.15 walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5, na watahiniwa 19,697 sawa na asilimia 48.41 walifaulu kwa kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 3.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, watahiniwa wenye ufaulu wa juu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Matumizi ya Sarufi* hususani mada ndogo ya *Ngeli za Nomino*. Watahiniwa hao waliweza kutumia mifano kutoa hoja mbili sahihi zenye kuonesha ubora na hoja tatu kuonesha udhaifu wa uainishaji wa ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimamboleo. Ubora wa kuanisha ngeli za nomino kimapokeo ni kama vile (i) *kusaidia kuondoa utata kwenye nomino zenye maana zaidi ya moja*, (ii) *kusaidia kuweka nomino zenye tabia moja kisintaksia katika ngeli moja*, (iii) *husaidia kutumia lugha kwa usahihi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi* na (iv) *husaidia kuthibitisha ubantu Kiswahili kwa kutumia kigezo cha kisintaksia*.

Aidha, udhaifu wa kuainisha ngeli kimapokeo ni pamoja na (i) *baadhi ya nomino zisizo na maumbo ya umoja na wingi kukosa ngeli* mfano, *uji*, *maji* na *njaa*, (ii) *mwingiliano wa viambishi kwa baadhi ya ngeli* mfano, *ngeli ya 2, 6 na 7 zote huwa na kiambishi cha umoja* U-. (iii) *Kiambishi* YU *cha ngeli ya kwanza ni cha kilahaja kisichoakisi Kiswahili sanifu* (iv) *Uanishaji wa ngeli hujikita katika viambishi awali vya vitenzi badala ya*

*nomino ambazo ndio msingi wa uanishaji ngeli* na (v) *Uanishaji hutumia viwakilishi vya mahali katika ngeli ya 9 badala ya nomino.* Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.

2. Kuanisha ngeli za nomino ni kitendo cha kuweka nomino katika ngeli au kundi linalofaa. Uanishaji wa ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimamboleo una ubora na udhaifu wake na ufuatao ni ubora wake.

Ubora

i/ Husaidia katika upatanisho wa kisarufi

Mfano: Kiti kimevunjika
Viti vimevunjika (KI-VI)

·Mtoto analia
Watoto wanalia (YU-A/WA)


hivyo uanishaji huu husaidia katika upatanisho wa kisarufi

ii/ Husaidia kuondoa utata katika maneno

Mfano: Paa ameruka juu
Paa wameruka juu (YU-A/WA)

Paa limeezekwa
Mapaa yameezekwa (LI-YA

huweza kuonesha tofauti katika maneno yanayofanana na kuondoa utata.



2: Udhaifu

iii/ Baadhi ya nomino hukosa ngeli
Mfano: Sukari
: Unga
Nomino hizi hukosa ngeli.

iv/ Baadhi ya viambishi vya ngeli hujirudia rudia
Mfano U-I Ngeli ya 2
U-ZI Ngeli ya 6
U-YA Ngeli ya 7
kiambishi U kimejirudia rudia katika ngeli hizi.

v/ Kiambishi YU katika Ngeli ya kwanza YU-A/WA ni cha kilahaja na si kiswahili sanifu
Mfano: YU-A/WA
kiambishi hiki si kiswahili sanifu

**Kielelezo Na. 2.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 2

Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili kwa kutoa hoja mbili sahihi za ubora na hoja tatu sahihi za udhaifu wa uainishaji wa ngeli za majina kwa mtazamo wa kimamboleo.


Kadhalika, asilimia 20.15 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 3.3 hadi 5.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kutoa hoja zisizojitosheleza katika kuonesha ubora na udhaifu wa kuainisha ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimamboleo. Baadhi yao walitoa hoja sahihi mbili hadi tatu kati ya hoja tano zinazoonesha ubora na udhaifu wa uainishaji wa ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimamboleo. Vilevile, watahiniwa wengine katika kundi hili walitoa hoja sahihi lakini walishindwa kutoa mifano inayoakisi hoja walizotoa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia mifano na kutoa hoja

mbili sahihi zinazonesha udhaifu wa uainishaji huu kama vile; (i) *Ngeli ya* PA- MU- KU *imejikita katika kuonesha mahali* na (ii) *Baadhi ya maneno hayana ngeli* mfano, *maji*. Vilevile, alitoa hoja ya (iii) kuwa, *baadhi ya ngeli hazipo katika ngeli za nomino* lakini alitoa mifano isiyo sahihi hivyo, kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, asilimia 48.41 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa umahiri kuhusu mada ndogo ya *Ngeli za Nomino*. Baadhi yao walijibu kwa usahihi hoja moja au mbili pekee. Watahiniwa wengine walitoa hoja bila kutoa mifano kwa kila hoja kama swali lilivyowataka. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliorodhesha ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimapokeo na kutoa mifano ya ngeli hizo bila kuonesha ubora wala udhaifu wa ngeli hizo kama swali lilivyomtaka. Mtahiniwa huyo aliandika;

Ngeli ya A – WA - *Huonesha umoja na wingi wa viumbe hai*
Mfano, *Mtoto – Watoto*

Hata hivyo, mfano aliotoa ni uainishaji wa ngeli kwa mtazamo wa kimapokeo, ambao huchunguza maumbo ya umoja na wingi ya nomino na si mtazamo wa kimamboleo unaojishughulisha na upatanisho wa kisarufi kwa kuangalia viambishi vya nomino katika vitenzi. Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuonesha ubora na udhaifu wa kuanisha ngeli kwa mtazamo wa kimamboleo na kupata 0.


02 Ubora
(i) Hufuata mtiririko sahihi
(ii) Huwa na Vionjo mbalimbali.
Udhaifu.
(i) Mara nyingi humupotosha msomaji
(ii) Huwa na misamiati michache
(iii) mtazamo huu hauvuti hisia za msomaji


**Kielelezo Na. 2.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 2

Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili kwa kutoa hoja zisizohusiana na ubora na udhaifu wa uainishaji wa ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimamboleo. Badala yake ametoa hoja za ubora na udhaifu zinazohusiana na uandishi wa insha kinyume na matakwa ya swali.

### 2.1.1.3 Swali la 3: Matumizi ya Sarufi

Swali lilitoka katika Mada ya *Matumizi ya Sarufi*, mada ndogo ya *Uundaji wa Maneno*. Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. Swali lilikuwa na vipengele viwili, ambapo mtahiniwa alitakiwa katika kipengele (a) kutoa sababu tano za watumiaji wa lugha ya Kiswahili kuunda maneno; na (b) kutaja maneno mawili yaliyoundwa kwa njia zifuatazo: (i) *Mpangilio wa fonimu*, (ii) *Kuunganisha maneno*, (iii) *Kutohoa kutoka lugha nyingine*, (iv) *Kufananisha umbo la kitu* na (v) *Tanakali sauti*.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 40,688 sawa na asilimia 100 ya wote waliofanya mtihani huu. Uchambuzi unaonesha kuwa, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani watahiniwa 36,853 sawa na asilimia 90.57 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3*

Katika Chati Na. 4, watahiniwa 20,607 sawa na asilimia 50.64 walifaulu vizuri kwa kupata alama 6 hadi 10, watahiniwa 16,246 sawa na asilimia 39.93 walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5, na watahiniwa 3,835 sawa na asilimia 9.43 walifaulu kwa kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 3.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, asilimia 50.64 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu walijibu vizuri swali hili na kupata ufaulu wa juu kuanzia alama 6 hadi 10. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuwa na umahiri wa kutosha kuhusu mada ndogo ya *Uundaji wa Maneno.* Watahiniwa hao walitoa sababu tano sahihi zinazowafanya watumiaji wa lugha ya Kiswahili kuunda maneno katika kipengele (a) kama vile; (i) Kuibuka kwa mambo mapya katika jamii na shughuli mbalimbali za kiuchumi, kisayansi, kiafya kisiasa na kiutamaduni. (ii) Kuongezeka na kupanuka kwa maendeleo ya teknolojia za habari na mawasiliano hivyo kuingiza istilahi nyingi ambazo hazikuwepo katika lugha ya Kiswahili. (iii) Kukidhi haja ya mawasiliano ya kila siku katika nyanja mbalimbali. (iv) Kukuza lugha ili kukidhi mahitaji ya jamii katika maeneo mbalimbali na (v) Kurahisisha mawasiliano kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili.

Aidha, katika kipengele (b) walitaja kwa usahihi maneno mawili sahihi kwa kila njia ya uundaji wa maneno kati ya njia tano walizopewa kama vile (i) **Mpangilio tofauti wa fonimu** - *Ona* na *noa*, (ii) **Kuunganisha maneno** - *Mwanamapinduzi;* linaloundwa na maneno *Mwana + mapinduzi* au *Mwanamuziki;* linaloundwa na maneno *Mwana + muziki*, (iii) **Kutohoa kutoka lugha nyingine** kama vile, *Shati* na *Baiskeli* yaliyotoholewa kutoka lugha ya Kiingereza, (iv) **Kufananisha umbo la kitu** kama vile *Kifaru - zana za kivita* na *Kidole tumbo - sehemu ya utumbo mpana inayofanana na umbile la kidole* na (v) **Tanakali sauti** – *Pikipiki*, neno linalotokana na sauti ya chombo hicho. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kukidhi matakwa yote ya swali.

| | | |
|---|---|---|
| 08 | @ Watumiaji wa lugha ya Kiswahili huunda | |
| | maneno kwa sababu | |
| | i) kukidhi haja ya mawasiliano | |
| | - Mfano uundaji wa maneno kama Sharubati | |
| | na Vibanzi | |
| | ii) Kwa sababu ya maendeleo ya sayansi | |
| | na Teknolojia | |
| | mfano maneno kama simu, Tarakilishi na | |
| | kinyonyi. | |
| | | |
| | iii) Huunda kwa lengo la kukuza lugha | |
| | - Lugha kukua ni kuongezeka kwa msamiati | |
| | hivyo maneno kama Safari Kinyonyi hukuza lugha | |



03 (a) i) Upungufu wa istilahi
- kwa sababu ya upungufu wa istilahi za kiswahili watu huamua kukopa maneno kutoka lugha zingine
mfano Shati - kiingereza
Kigoda - kigogo
Leso - kireno

ii) Lakini pia watu huunda maneno kwa lengo la kuficha maana ya jambo au usiri
mfano maneno yanayoundwa kwa kubadili maana ya msingi na msimu
mfano Demu - (Buzwagi) mwanamke wa watu wote
Kisu - Mwanamke mzuri
Chupa - Sururi inayobana.

03 (b) i) Mpangilio tofauti wa fonimu
- Huu ni uundaji wa kuchukua fonimu zinazo fanana kuunda maneno tofauti
mfano:- IMLA mfano 2: UVUM
LAMI UMVU
MILA

ii) kuunganisha maneno
mfano, Askari kanzu
Mbwa mwitu

iii) kutohoa kutoka lugha nyingine
mfano Shati - kiingereza
Demokrasia - kigiriki

iv) kufananisha umbo la kitu
mfano;- kifaru - mnyama waporini umbo lake linafananishwa na gari la jeshi la vita kubwa

(b) v) kiiiko :- Gari kubwa linalotumika katika shughuli za ujenzi lenye kijiko mbele.

b) vi) Tanakali sauti
mfano:-Pikipiki - mlio wa chombo cha usafiri chenye matairi mawili
Malapa - Aina ya viatu vitumiwa na mtu na kutembea huita hivyo.

**Kielelezo Na. 3.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 3


Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi vipengele vyote viwili vya swali hili kwa kutoa sababu tano sahihi zinazowafanya watumiaji wa lugha ya Kiswahili kuunda maneno katika kipengele (a) na kutaja kwa usahihi maneno mawili sahihi kwa kila njia ya

uundaji wa maneno katika njia zote tano alizopewa na kupata alama zote 10.

Aidha, asilimia 39.93 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa vingine. Baadhi yao katika kipengele (a) walitoa sababu moja hadi mbili sahihi za kuunda maneno ya lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa sababu sahihi ya (i) *kukuza lugha*; lakini alitoa sababu nyingine nne zisizo sahihi kama vile; (ii) *kueneza lugha*, (iii) *kwa ajili ya misimu*, (iv) *umri* na (v) *utengano wa kijiografia*, ambapo sababu ya (ii) inahusiana na ukuaji na ueneaji wa lugha ya Kiswahili; (iii) misimu ni maneno yasiyo sanifu yanayozuka na kupotea na yanayodumu husanifishwa na kuingizwa kwenye msamiati wa lugha; (iv) ni jambo la kuzingatia katika matumizi ya lugha na (v) ni moja ya sababu ya kutokea kwa lahaja mtawalia. Majibu hayo yalimfanya mtahiniwa huyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, asilimia 9.43 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa umahiri wa mada ndogo ya *Uundaji wa Maneno*. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili katika kipengele (a) walitoa sababu za uundaji wa maneno zisizo sahihi kama vile; (i) *upatanisho wa kisarufi* ambao ni mtazamo wa kimamboleo katika uainishaji wa ngeli za nomino; (ii) *mpangilio wa konsonanti*, ambazo ni moja ya sauti za lugha zinazotamkwa kwa kuwepo na kizuizi cha hewa kutoka mapafuni; (iii) *kuunganisha maneno* na (iv) *tanakali sauti*, ambazo ni njia za uundaji wa maneno na (v) *sababu ya kikamusi* ambazo kwa ujumla sio sababu za uundaji wa maneno kama swali lilivyotaka.

Katika kipengele (b), watahiniwa hao walishindwa kutaja maneno mawili kwa kila njia walizopewa badala yake baadhi walitunga sentensi kwa kutumia njia hizo kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitunga sentensi kupitia njia zifuatazo: (ii) Kuunganisha maneno *Dada <u>ni</u> mkali*, (v) Tanakali sauti - *Mama* – (*ma-ma*) na *Baba* – (*ba-ba*). Hivyo, kupata 0. Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili na kupata alama hafifu.



03 (a) i/ huunda maneno ili kueleza vitenzi
Mfano:- piga
ii/ Ili kueleza mahali
Mfano: shuleni
- Juma anaenda shuleni kila siku
iii/ Huunda maneno ili kueleza nomino
Mfano:- Baba
- Baba analima
iv/ Huunda maneno ili kuelezea kiwakilishi
Mfano yule
- Yule ni mrefu sana
v/ Huunda maeneno ili kuelezea yambwa
Mfano: pigwa
Hamisi amepigwa na Chuma.
(b) i/ Som - soma.
Som - somi.
ii/ Baba na mama wanasali
anacheza kama anajua.
iii/ Sahani
- lugha.
iv/ Paa ni kubwa kama wingu
- Amina ni mwembamba kama sisimizi
v/ Kaa! Kaa!
paa! paa!

**Kielelezo Na. 3.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 3

Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu mseto yasiyohusiana na sababu za watumiaji wa lugha ya Kiswahili kuunda maneno. Katika kipengele (a) alibainisha aina za maneno (*vitenzi, nomino, viwakilishi*) na kutaja maneno yasiyohusiana na njia za uundaji wa maneno alizopewa katika kipenge (b), hivyo kupata 0.

### 2.1.1.4 Swali la 4: Utumizi wa Lugha

Swali hili lilitoka katika mada ya *Tafsiri na Ukalimani* na mada ndogo ya *Tafsiri*. Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kutafsiri sentensi za Kiswahili alizopewa kwenda lugha ya Kiingereza. Swali lilimtaka

mtahiniwa kutafsiri sentensi alizopewa katika lugha ya Kiingereza kwa kuzingatia tafsiri ya kisemantiki. Swali liliuliza;

> *Tafsiri sentensi zifuatazo katika lugha ya Kingereza kwa kuzingatia tafsiri ya kisemantiki.*
>
> (i) *Mwaka jana, Rais alizindua kampeni ya kudhibiti malaria.*
> (ii) *Jana nilimtembelea mjomba wangu.*
> (iii) *Ili ufanikiwe, ni lazima uwe na uwezo wa kufanya maamuzi.*
> (iv) *Nilipokea taarifa kwamba baba yangu amenunua nyumba mpya.*
> (v) *Hivyo ndivyo timu ya Taifa ilivyoshindwa.*
> (vi) *Ninawachukia watu wanaowasumbua wengine.*
> (vii) *Asili ya lugha ya Kiswahili inavutia sana.*
> (viii) *Tutakwenda shule ya Sekondari Mtakuja kwa ajili ya mashindano ya mdahalo.*
> (ix) *Tafadhali! Nipatie nakala ya wasifu wako binafsi.*
> (x) *Tunakaribia kumaliza mitihani yetu.*

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 40,688 sawa na asilimia 100 ya wote waliofanya mtihani huu. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani ambapo, watahiniwa 20,472 sawa na asilimia 50.31 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Jedwali Na. 2 linaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

**Jedwali Na. 2: Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa**

| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0 – 3.0 | 20,216 | 49.69 |
| 3.5 - 5.5 | 9,893 | 24.31 |
| 6.0 -10 | 10,579 | 26.00 |

Katika Jedwali Na. 2, watahiniwa 10,579 sawa na asilimia 26.00 walikuwa na ufaulu wa juu kuanzia alama 6 hadi 10, watahiniwa 9,893 sawa na asilimia 24.31 walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5, na watahiniwa 20,216 sawa na asilimia 49.69 walifaulu kwa kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 3.

Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa, takriban nusu yao yaani asilimia 49.69 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3. Ufaulu huu hafifu ulitokana na watahiniwa hao kukosa umahiri katika mada ya *Tafsiri na Ukalimani* hususani mada ndogo ya *Tafsiri ya Kisemantiki*. Asilimia 12.00 ya watahiniwa hao walionesha kutokuwa na uelewa wa kutosha wa lugha ya Kiingereza na kushindwa kumudu sarufi ya lugha hiyo. Baadhi yao waliandika maneno yasiyo sanifu ya lugha ya kiingereza na wengine walitafsiri kwa usahihi sentensi moja hadi tatu kati ya sentensi kumi walizopewa, hivyo kupata alama hafifu 1 hadi 3.

Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kabisa kutafsiri kwa usahihi sentensi zote kumi alizopewa kwa kutumia tafsiri sisisi kama vile (i) *Last year, President open the malaria campaign committee yenye* maana ya **Mwaka jana, Rais alifungua baraza la kampeni ya malaria** kinyume na maana halisi ya sentensi aliyopewa yaani ‘Mwaka jana, Rais alizindua kampeni ya kuthibiti malaria’ ambapo alitakiwa kuitafsiri sentensi hiyo kisemantiki kama ifuatavyo: *Last year, the president launched a campaign to control malaria*. Kadhalika, katika kipengele (iii) aliandika *If you must won, you must be able to do decide* yenye maana ya **Kama lazima ulishinda, lazima uweze kufanya maamuzi** kinyume na maana halisi ya sentensi aliyopewa yaani ‘Ili ufanikiwe, ni lazima uwe na uwezo wa kufanya uamuzi’ ambapo alitakiwa kuitafsiri kama ‘*To succeed, you must be able to make decisions*.’ Kwa ujumla watahiniwa walitakiwa kutafsiri sentensi walizopewa kwa kuzingatia tafsiri ya kisemantiki kama ifuatavyo:

(i) *Mwaka jana, Rais alizindua kampeni ya kudhibiti malaria.* (Last year, the President launched/inaugurated anti-malaria campaign/Last year, the President launched/inagurated a campaign to control malaria).

(ii) *Jana nilimtembelea mjomba wangu.* (Yesterday I visited my uncle).

(iii) *Ili ufanikiwe, ni lazima uwe na uwezo wa kufanya maamuzi.* (To succeed, you must be able to make decisions/For you to succeed, you must have the ability to make decisions).

(iv) *Nilipokea taarifa kwamba baba yangu amenunua nyumba mpya.* (I received the information that my father has bought new house).

(v) *Hivyo ndivyo timu ya taifa ilivyoshindwa.* (That is how national team got defeated/ That is how the national team lost/failed).

(vi) *Ninawachukia watu wanaowasumbua wengine*. (I hate people who disturb others.)

(vii) *Asili ya lugha ya Kiswahili inavutia sana*. (The origin of Swahili language is very interesting/amazing).

(viii) *Tutakwenda Shule ya Sekondari Mtakuja kwa ajili ya mashindano ya mdahalo.* (We will go to Mtakuja Secondary School for a debate competition).

(ix) *Tafadhali! Nipatie nakala ya wasifu wako binafsi.* (Please, give me a copy of your Curriculum Vitae).

(x) *Tunakaribia kumaliza mitihani yetu.* (We are about to finish our examinations.)

Kielelezo Na**.** 4.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili na kupata alama 0.

04. (i) Mwaka jana, Rais alizindua kampeini ya kuthibiti malaria

-> Last year president introduced the policy to Fought against malaria

(ii) Jana nilimtembelea mjomba wangu

-> Yerstaday

-> Yerstadey I visted my uncle


-> He Visted my uncle Yerstaday

(iii) Ili ufanikiwe ni lazima uwe na uwezo wa kufanya uamuzi

-> Your ~~sucess~~ success depend on good decision

(iv) Nilipokea taarifa kuwa baba yangu amenunua nyumba mpya

-> My Father was ~~ff~~ bought a new house I got information



04. (i) Hivyo ndivyo timu ya Taifa ilivyo shindwa!
→ How nation team was prove Failure

(vi) Ninawachukia watu wanao wasumbua wengine
→ We must not distable Others

(vii) Asili ya lugha ya Kiswahili inavutia
→ Nature of Kiswahili languag e are show good visual impression

(viii) Tutakwenda shule ya sekondari Mtakuja kwa ajili ya majadiliano ya mdahalo
→ Were They will visit at mtakuja sekondari For the aim of Debate

(ix) Tafadhari! Nipatie nakala ya wasifu wako binafsi
→ Sorry! give me your culumlam vitae (CV)


(x) Tunakaribia kumaliza mitihani yetu
→ were in the way to Finish our examination

**Kielelezo Na. 4.1**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 4

Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutafsiri sentensi zote alizopewa katika lugha ya Kiingereza kwa kuzingatia tafsiri ya kisemantiki.

Kwa upande mwingine, asilimia 26.00 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu walijibu vizuri swali hili na kuwa na ufaulu wa juu kuanzia alama 6 hadi 10. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Tafsiri na Ukalimani* hususani mada ndogo ya *Tafsiri*. Watahiniwa hao walipata alama za juu 6 hadi 9, kutokana na kujibu kwa usahihi sentensi nyingi na kushindwa kutafsiri sentensi chache. Watahiniwa wengi katika kundi hili walishindwa kutafsiri kwa usahihi sentensi ya (i) kwa kushindwa kutafsiri neno *kuzindua* ambalo kwa

kiingereza ni **launched** au **inaugurated** badala yake walitumia msamiati *established* wenye maana ya **kuanzisha**. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alionesha kuwa na umahiri wa hali ya juu wa lugha ya Kiingereza, hivyo kuweza kutafsiri kwa usahihi sentensi zote kama Kielelezo Na. 4.2 kinavyodhihirisha:



Tafsiri kwenda kwa lugha ya Kiingereza kwa tafsiri ya kisemantiki

4\. i) Last year the president launched a campaign to control malaria.

ii) Yesterday, I visited my uncle.

iii) To succeed, you must have ability to make decision.

iv) I received information that my father has bought new house.

v) That's how the national team failed.

vi) I hate people who disturb others.

vii) The origin of Kiswahili language is very amusing.

viii) We will go to Mtakuja Secondary school for debate competition

ix) Please! Give me your Curriculum Vitae.

x) We are nearly to finish our examinations.

**Kielelezo Na. 4.2**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 4

Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetafsiri kwa usahihi na kupata alama za juu katika swali hili licha ya kuwa na mapungufu madogo madogo ya kitahajia.

Kadhalika, asilimia 24.31 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 3.3 hadi 5.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kutafsiri kwa usahihi baadhi ya sentensi na kushindwa kutafsiri sentensi nyingine kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza kwa kuzingatia tafsiri ya kisemantiki. Baadhi yao walitafsiri kwa usahihi sentensi tatu hadi sita kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa tafsiri sahihi katika vipengele (ii) *I visited my uncle yesterday*, (iv) *I recieved information that my father bought a new house*. (v) *That is how the national team defeated*. (vi) *I hate people who disturb others* na (viii) *We will go to Mtakuja secondary school for debate competition*.

Kwa upande mwingine, mtahiniwa huyo alitafsiri isivyo sentensi nyingine tano kama vile; (i) *The president introduced anti – malaria compaign last year*. (iii) *In order to benefit you must have ability to take action* yenye maana ya **Ili unufaike lazima uwe na uwezo wa kuchukua hatua**. (vii) *The nature of Kiswahili language is very interesting* yenye maana ya **Asili ya Kiswahili inavutia sana** japo neno *nature* huzungumzia *uoto* na sio asili inayotumika kwa lugha. (ix) *Xorry! Give me a copy of Curriculum Vitae* yenye maana ya **Nipe nakala ya wasifukazi** ambapo neno *xorry* ni neno lisilo na maana katika lugha ya Kiingereza. Mtahiniwa huyo alitakiwa kutumia neno sahihi **sorry** lenye maana ya samahani. Pia, katika kipengele (x) aliandika *We are approaching to end our exams* akimaanisha **Tunakaribia kufika mwisho wa mitihani yetu**; majibu ambayo hayakujitosheleza, hivyo kupata alama za wastani.

### 2.1.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAREFU


Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali manne ya insha. Swali la tano (5) lilikuwa ni la lazima. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu na kila swali lilikuwa na alama 20.

#### 2.1.2.1 Swali la 5: Utungaji

Swali hili lilitoka katika mada ya *Utungaji* hususani mada ndogo ya *Wasifukazi* na lililenga kupima uundaji. Swali hili lilikuwa la lazima na

lilimtaka mtahiniwa akiwa kama mhitimu wa Shahada ya Ualimu kutoka Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam kuandika wasifukazi atakaotuma kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuomba nafasi kazi ya Ualimu wa Sekondari kutokana na tangazo la lililotolewa na Wizara hiyo. Jina lake liwe Sabini Tanu Ishirini.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa, swali hili lilijibiwa na watahiniwa 40,688 (100%) waliofanya mtihani. Swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri ambapo watahiniwa 38,465 sawa na asilimia 94.54 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama 7 hadi 20. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 5**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Katika Chati Na. 5, watahiniwa 25,446 sawa na asilimia 62.54 walikuwa na ufaulu mzuri kuanzia alama 12 hadi 20, watahiniwa 13,019 sawa na asilimia 32.00 walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5, na watahiniwa 2,223 sawa na asilimia 5.46 walifaulu kwa kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5.

Watahiniwa wengi waliojibu swali hili, asilimia 62.54 walikuwa na ufaulu mzuri kwa kupata alama kuanzia alama 12 hadi 20. Miongoni mwao, asilimia 13.29 walifanya vizuri zaidi na kupata alama za juu kuanzia 16 hadi 20. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuwa na maarifa ya kutosha juu mada ya *Utungaji* hususani mada ndogo ya *Uandishi wa Wasifukazi*. Watahiniwa wengi katika kundi hili walionesha kuwa na

umahiri wa kutosha katika uandishi wa wasifukazi hivyo waliweza kuandika wasifukazi mzuri kwa kuzingatia muundo sahihi wa uandishi wa wasifukazi kama vile kichwa cha wasifukazi kilichoandikwa kwa herufi kubwa, taarifa binafsi zinazoonesha jina kamili, tarehe ya kuzaliwa, uraia, lugha mahali alipozaliwa, hali ya ndoa, jinsi, anuani yaani sanduku la barua, anuani ya barua pepe na namba ya simu. Vilevile, watahiniwa hao waliweza kuandika usuli wa kielimu yaani ngazi za kielimu au na mafunzo waliyopitia, uzoefu wa kazi, ujuzi mbalimbali walio nao na majina ya wadhamini wawili pamoja na anwani zao.

Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika wasifukazi kwa kuzingatia muundo sahihi kama vile; Kuandika kichwa cha wasifukazi kwa herufi kubwa - *WASIFUKAZI*, kuandika taarifa zake binafsi *Usuli wa kielimu*, ambapo alichora jedwali linaloonesha ngazi ya juu ya elimu mpaka ya chini na kuonesha miaka aliyopata elimu hiyo na vyeti alivyotunukiwa katika ngazi hizo za elimu. Pia, alionesha uzoefu alionao wa kazi aliyoomba, *ujuzi wa kompyuta na udereva*. Vilevile, aliandika mambo anayopendelea kuwa ni *kucheza mpira wa miguu* na *kusoma* vitabu; pia aliandika majina mawili ya wadhamini. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa katika kundi hili waliandika wasifukazi uliokuwa na mapungufu madogo madogo kama vile; kutokuandika sanduku la posta, lugha wanazozungumza, uraia na mengineyo. Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili kwa kukidhi matakwa yote ya swali.

5. WASIFU KAZI.

A. TAARIFA BINAFSI.

Jina: Sabini Tanu Ishirini.

Uraia: Mtanzania

Jinsi: Me

Mwaka wa Kuzaliwa (Tarehe): 27 Aprili, 2000

Lugha: Kiswahili, Kingereza na Kifaransa.

Anuani: S.L.P 147,

Barua Pepe: sabini20tanu@yahoo.com.

Mawasiliano: 0764286662

Mahali pa kuzaliwa: Ilemela Mwanza.

Mahali pa kuishi: Arusha.


B. USULI WA ELIMU.

| MWAKA | NGAZI YA ELIMU / TAASISI | TUZO. |
|---|---|---|
| 2020-2024 | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. | Shahada ya Ualimu |
| 2019-2020 | Shule ya Sekondari Kisimiri - Arusha | Cheti cha elimu ya upili (Sekondari) |
| 2015-2018 | Shule ya Sekondari Mwanza - Mwanza | Cheti cha elimu ya Sekondari (kidato cha nne). |

| MWAKA | TAASISI /NGAZI YA ELIMU | TUZO |
|---|---|---|
| 2008 - 2014 | Shule ya msingi Migombani - Mwanza | Cheti cha elimu ya msingi |

C. UZOEFU WA KAZI

| MWAKA | KAMPUNI / TAASISI | CHEO |
|---|---|---|
| 2024-2025 | Shule ya Sekondari Maria - Dar es Salaam | Mwalimu wa Kujitolea. (somo la Hisabati). |
| 2025- | Shule ya Sekondari Kibambati - Pwani | Mwalimu wa Kujitolea (somo la Fizikia). |



D. ASHKI /MAPENDELEO.
i) Kusoma na kuandika vitabu.
ii) Kukimbia riadha.
iii) Kucheza mpira wa gofu.
iv) Kuimba.

E. STADI /UJUZI.
i) Kuzungumza lugha ya kiswahili na kingereza.
ii) Kutunga mashairi.
iii) Ujuzi katika TEHAMA.
iv) Ujuzi katika masuala ya ujasiriamali.

F. WADHAMINI.
a) JOHN C. NUNGWANA,
Mhadhiri Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,
S.L.P 1140,
Dar es Salaam,
john26@gmail.com
0764171722

b) ARSON J. LEMA,
Mkuu wa Shule ya Sekondari Mwanza,
S.L.P 2617,
Mwanza.
lemaarson@yahoo.com.

c) LIZBETH F. ISAEL,
Mkemia Mkuu TMDA,
S.L.P 1104,
Arusha
isaelfaustinelizy@gmail.com
0674171204


**Kielelezo Na. 5.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 5

Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika wasifukazi kwa kuzingatia muundo sahihi wa wasifukazi na kupata alama za juu 19.

Aidha, asilimia 32.00 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata ufaulu wa wastani kuanzia alama 3.3 hadi 5.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuandika wasifukazi ambao unakidhi baadhi ya matakwa

ya uandishi kama vile; kichwa cha wasifukazi, taarifa binafsi zinazoonesha jina kamili, tarehe ya kuzaliwa, uraia, lugha mahali alipozaliwa, hali ya ndoa, jinsi, anuani yaani sanduku la barua, anuani ya barua pepe na namba ya simu, usuli wa kielimu yaani ngazi za kielimu au na mafunzo waliyopitia, uzoefu wa kazi, ujuzi mbalimbali walio nao na majina ya wadhamini wawili pamoja na anwani zao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika wasifukazi bila kuzingatia jina alilopewa na taarifa nyingine kama vile j*insi*, *anuani* sanduku la posta, *tarehe ya kuzaliwa* na *hali ya ndoa*. Vilevile, mtahiniwa mwingine aliandika mambo anayopendelea ni *shule kuwa na nyumba za walimu karibu na maeneo ya shule* badala ya mambo kama kusoma vitabu au kucheza mpira, hivyo, kupata alama za wastani 12.

Hata hivyo, asilimia 5.46 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu walijibu vibaya swali hili na kupata ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 5.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa umahiri kuhusu mada ya *Utungaji* hususani mada ndogo ya *Uandishi wa Wasifukazi*. Miongoni mwao wapo walioandika wasifukazi bila kuzingatia muundo sahihi wa uandishi hususani kichwa cha wasifukazi, taarifa binafsi, usuli wa kielimu, uzoefu wa kazi, ujuzi mbalimbali walio nao na majina ya wadhamini. Kutokana kukosa umahiri huo, baadhi ya watahiniwa waliandika vifungu vya insha na wengine waliandika barua ya kikazi kutokana na kuchanganya wasifukazi na barua ya maombi ya kazi. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili na kupata alama 0.



5.

CHUO KIKUU,
S. L. P 40,
DAR-ES-SALAAM
06 - 05 - 2025

KATIBU MKUU,
WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA,
S. L. P 30,
DAR-ES-SALAAM.

Ndugu,

YAH: OMBI LA KAZI YA UALIMU KATIKA ELIMU YA SEKONDARI

Tafadhari husika na kichwa cha habari hapo juu.

Mimi ninaitwa Sabini T. Ishirini ni mhitimu wa shahada ya ualimu kutoka chuo kikuu cha Dar-es-Salaam. Ninaomba kazi ya ualimu wa sekondari.

Nitashukuru iwapo ombi langu litakubalika

Wako mtiifu

Ishirini

SABINI TANU ISHIRINI


**Kielelezo Na. 5.2**: Sampuli ya Jibu lisilo Sahihi katika Swali la 5

Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika barua ya kuomba kazi ya ualimu kinyume na muundo wa uandishi wa wasifukazi na kupata 0.

### 2.1.2.2 Swali la 6: Maendeleo ya Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili*, mada ndogo ya *Kukua na Kuenea kwa Kiswahili*. Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutathmini shughuli mbalimbali zilizofanywa na wakoloni nchini Tanzania zilizosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri sana ambapo watahiniwa 39,890 kati ya 40,688 walilijibu. Kati yao, watahiniwa 39,817 sawa na asilimia 99.82 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 7 hadi 20 kama inavyoonekana katika Chati Na. 6.





**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Katika Chati Na. 6, watahiniwa 36,198 (90.74%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20, watahiniwa 3,619 (9.08%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5, na watahiniwa 73 (0.18%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi (90.74%) walijibu vizuri swali hili na kupata alama kuanzia 12 hadi 20. Kati yao, asilimia 38.05 walifaulu vizuri na kupata alama za juu 16 - 20 kwa kuwa waliweza kufafanua kwa usahihi mchango wa wakoloni katika harakati za kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania.


Aidha, watahiniwa hao walifafanua shughuli sita zilizofanywa na wakoloni nchini Tanzania na kuonesha jinsi zilivyosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili kama vile shughuli za kidini ambapo lugha ya Kiswahili ilitumika kutolea mafundisho yote ya dini ya Kikristo na ya Kiislamu; shughuli za kiuchumi ambapo shughuli za kilimo na za kibiashara zilifanywa na watanzania kutoka makabila mbalimbali ambao waliunganishwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili; shughuli za kiutawala/mahakama, wakoloni waliwaajiri maakida, matarishi na maafisa wengine wa ngazi za chini waliokuwa na ujuzi wa lugha ya Kiswahili ili kusimamia utekelezwaji wa sheria na sera za utawala wao; shughuli za kielimu, wakoloni walianzisha shule ili watu wajifunze Kiswahili kwa lengo la kupata wafanyakazi; shughuli za kijamii, wakoloni walitoa huduma za kijamii kama vile afya, usafiri na usafirishaji kwa lugha ya Kiswahili ili kurahisisha utawala wao; na shughuli za kiutamaduni zilizohusisha uchezaji wa muziki wa kigeni zilitumia lugha ya kiswahili.

Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swali hili.



06. Kiswahili, ni lugha inayotumika na wat-
u au wakazi wanaoishi katika mwambao w-
a Afrika ya mashariki na kati yenye kuj-
umuisha lahaja tofautitofauti kama lahaja
ya kiunguja, Kimtang'ata, Kiamu, Kimrima.
Kwa namna moja au nyingine wakoloni wameji-
tahidi sana katika kukuza na kueneza kiswah-
ili kutokana na sababu tofautitofauti. Zifuatazo
ni moja kueleza shughuli mbalimbali ambazo
wakoloni walizifanya katika kukuza na kue-
neza lugha ya kiswahili ;-
Shughuli za Kielimu, kwa kutumia eli-
mu katika ngazi tofautitofauti kulipelekea sana
kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili
kwa namna moja au nyingine ambapo wa-
koloni walijenga shule mbalimbali na kutoa e-
limu ya lugha ya kiswahili katika nchi ya
Tanzania mfano wa shule ni kama pugu,
peramiho na hata Tabora Boys ambapo lugha
ya kiswahili ilitumika kufundishia na hata
somo ya lugha pia kufundishwa hivyo sh-
ughuli ya elimu kutoka kwa wakoloni imes-
aidia sana katika kukua na kuenea kwa
lugha ya kiswahili.
Shughuli za kidini, pia kutokana k-
wa kukua na kuenea kwa dini mbalim-
bali kama kiislamu, kikristo ambapo ilikuw-
a mojawapo ya njia ya kuhimiza ukoloni,
wakoloni walitumia lugha ya kiswahili kati-
ka kukuza na kueneza dini. Mfano, Waar-
abu walitumia lugha ya kiswahili katika
kueneza dini ya Kiislamu hasa pwani ya
Afrika ya mashariki pia kutumia lugha ya
Kiswahili kutafsiri vitabu vya dini kama K-
urani na Biblia Takatifu, sana sana kwa
kutumia wamisionari ambao walijenga vituo
, kufanya tafsiri ilipelekea kukua na kuen.

06. ea kwa lugha ya kiswahili.
Shughuli za kibiashara, pia kutokana
na kufanya biashara mbalimbali kulipelekea
sana kukua na kuenea kwa lugha ya ki
wahili kwani lugha ni muhimu katika k
ufanikisha marungumo na kuhimiza maele-
wano katika kufanikisha shughuli mbalimb
ali za kibiashara. Mfano Waarabu walifa-
nya shughuli za kibiashara za kuuza na
kununua watumwa kupelekea lugha ya kiswa-
hili kufahamika kama lugha ya watumwa
na pia kupata maneno kama fedha, the-
luthi, kubadhi.
Shughuli za kiutawala, pia kutokan-
a na shughuli za kiutawala kulipelekea
sana kukua na kuenea kwa lugha ya
Kiswahili kwani katika ngazi fulani za kiuta-
wala hasa za chini kama maakida na
Jumbe walitumia lugha ya Kiswahili kati-
ka kuunganisha watawala na wanaotawali
wa. pia katika shughuli ya usanifishaji
ambayo ilifanywa na utawala wa waingereza
za kulipelekea pia kukua na kuenea ku
a lugha ya kiswahili.
Shughuli za mahakama, pia katik
a utawala wa wajerumani ulikuwa na shu
ghuli za kimahakama ambapo kwa namn
a moja au nyingine kulipelekea sana k
hafa kukua na kuenea kwa lugha ya kisw
ahili kwani kupitia matumizi yake ma-
pana katika kufanikisha kesi mbalimbali
na tofautitofauti kulikuwepo kupelekea sana


06. Kukua na kuenea kwa lugha ya kiswahili, hivyo shughuli za mahakama ni muhimu katika kukua na kuenea lugha ya kiswahili kipindi cha ukoloni.

Shughuli za kilimo au mashamba, pia katika utawala wa wakoloni, walikuwa na mashamba makubwa ambayo kwa namna moja au nyingine yalihusisha matumizi ya watumwa ambao ni waafrika hivyo katika kufanikisha shughuli mbalimbali za mashamba kulihitajika matumizi mapana ya lugha ya kiswahili. Hivyo kwa namna mbalimbali kiswahili kilitumika kusingi katika kufanikisha kazi na jukumu zima la kilimo cha mashamba hivyo ni mojawapo ya shughuli ambayo ilipeleka kukua na kuenea kwa lugha ya kiswahili nchini Tanzania.

Kwujumla, maendeleo ya lugha ya kiswahili hutokana na mambo mengi sana hata hivi leo kuna shughuli nyingi ambazo hupelekea kukua na kuenea kwa lugha ya kiswahili duniani kote kama elimu, biashara, utalii, mikutano ya kimataifa. Hivyo serikali inapaswa kufanya hima na jitihada mbalimbali katika kuhamasisha kukua na kuenea kwa lugha ya kiswahili na kuweza kufanya itumike na kuleta manufaa chanya katika jamii.

**Kielelezo Na. 6.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi Katika Swali la 6


Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua kwa usahihi shughuli sita zilizofanywa na wakoloni nchini Tanzania zilizosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili na kupata alama za juu.

Aidha, asilimia 9.08 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata ufaulu wa wastani kuanzia alama 7.0 hadi 11.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kufafanua kwa usahihi baadhi ya shughuli na kushindwa kufafanua kwa usahihi shughuli nyingine zilizofanywa na wakoloni nchini Tanzania zilizosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili. Miongoni mwao wapo walitoa hoja sahihi lakini ufafanuzi haukujitosheleza, hivyo kupata

alama za wastani. Pia, baadhi yao walifafanua kwa usahihi hoja kama vile; *biashara, kilimo, shughuli za kiutawala* na s*hughuli za utoaji wa huduma za kijamii* lakini maelezo yaliyotolewa hayakujitosheleza. Watahiniwa wengine walifafanua hoja ya *shughuli za mawasiliano na uchukuzi* na *uchimbaji wa madini* ambazo hazikuwa shughuli zilizofanywa na wakoloni katika kukuza na kueneza Kiswahili chini Tanzania bali zilisaidia katika mchakato huo baada ya uhuru, hivyo, kupata alama za wastani.

Pamoja na watahiniwa wengi kufanya vizuri na kupata alama za juu na wastani katika swali hili, watahiniwa wachache sawa na asilimia 0.18 walifanya vibaya na kuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa umahiri katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* kwa ujumla na mada ndogo ya *Kukua na kuenea kwa Kiswahili Nchini Tanganyika Kabla ya Uhuru*. Kutokana na kukosa umahiri huo, baadhi ya watahiniwa waliorodhesha wageni mbalimbali waliozuru Tanganyika wakati wa ukoloni na wengine walibainisha njia mbalimbali zilizotumiwa na wakoloni katika utawala wao bila kuhusisha shughuli zao zilizosaidia katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua shughuli za *kielimu*, *biashara* na *michezo* lakini ufafanuzi wake haukujitosheleza, hivyo kupata alama za chini. Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Wakoloni hawa ni watawala wa kutoka | |
| | uingereza walio tawala Tanganyika kabla haik- | |
| | upata Uhuru, wakoloni hawa walifanya mambo | |
| | mbalimbali yaliyofanya kiswahihili [sic] iweze kuk- | |
| | ua na hapa nchini Tanzania kipindi cha | |
| | utawala wao mfano walisanifisha kiswahi | |
| | li. Ifuatayo ni shughuli zilizofanywa na | |
| | wakoloni nchini Tanzania zilizo saidia | |
| | kukua na kuenea kwa kiswahili. | |
| | Wakoloni walifanya Usanifishaji wa | |
| | lugha ya kiswahili. Tangu kabla ya ujio | |
| | wa wakoloni kiswahili hakikupata nafasi. | |
| | ya kusanifishwa na wazawa wa lugha | |
| | hiyo hadi kipindi cha utawala wa | |
| | mkoloni mwaka 1925 ndipo shughuli ya | |
| | usanifishaji kilianza. | |
| | Wakoloni waliruhusu kiswahili | |
| | kutumika katika elimu za msingi kama | |
| | lugha ya kufundishia. Tangu kipindi cha | |
| | utawala wa mkoloni kiswahili kilitumika | |


6 katika kutolea elimu shule za msingi
na kingereza kutufundishwa kama somo.
Kuruhusu kiswahili kutumika katika
utawala hasa ngazi ya chini. katika utawa-
la kiswahili kilitumika kama lugha ya
kuwasiliana baini ya viongozi na wananchi
ambao walikuwa katika ngazi ya chini
kabisa katika utawala wa mkoloni.
Mkoloni aliunda kamati ya ukuzaji
na usanifishaji wa kiswahili. katika kipindi
cha utawala wa mkoloni ndipo shughuli
ya usanifishaji ili fanyika na hata
kuunda kamati ya kiswahili ambayo
ilifahamika kama The east Africa kiswahili
language committe.
Ujenzi wa miundo mbinu ambayo
ilisaidia kipindi cha usanifishaji. mkoloni
ndiye aliyejenga miundombinu ya kwanza
hapa nchini na ujenzi huo wa miundo
mbinu hiyo ni kama vile barabara na
reli, miundombinu hii ilitumiwa na
wasanifishaji.
wakoloni walianzisha shughuli za
umisionari nchini. Shughuli hizi za umision-
anari ilichangia kwa sehemu kubwa
kukua na kuenea kwa kiswahili nchini
kipindi cha utawala wao hivyo shughuli
hizi za umisionari pia ili changia kukua
na kuenea kwa kiswahili.

**Kielelezo Na. 6.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Katika Swali la 6


Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua shughuli zisizo sahihi katika hoja ya nne na ya tano. Pia, hoja ya kwanza na ya sita hazikuwa na ufafanuzi uliojitosheleza kwani hakuonesha namna shughuli hizo zilizofanywa na wakoloni zilivyosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania.

### 2.1.2.3 Swali la 7: Maendeleo ya Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* hususani mada ndogo ya *Usanifishaji wa Lugha ya Kiswahili*. Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kubaini hatua muafaka za usanifishaji na

lilimtaka mtahiniwa kueleza hatua tano zilizofanywa na serikali ya Waingereza katika usanifishaji wa lugha ya Kiswahili.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 35,040 (86.10%) kati ya 40,688 waliofanya mtihani huu. Swali hili lilijibiwa vizuri ambapo, watahiniwa 34,394 sawa na asilimia 98.16 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 7 hadi 20. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Katika Chati Na. 7, watahiniwa 29,470 sawa na asilimia 84.10 walikuwa na ufaulu wa kiwango cha juu kuanzia alama 12 hadi 20, watahiniwa 4,924. sawa na asilimia 14.05 walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 14, na watahiniwa 646 sawa na asilimia 1.85 walifaulu kwa kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa asilimia 84.10 ya walijibu vizuri swali hili na kupata ufaulu wa juu kuanzia alama 12 hadi 20. Miongoni mwao, watahiniwa 9,618 sawa na asilimia 27.45 walijibu vizuri zaidi swali hili na kupata alama za juu 17 hadi 20. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuonesha kuwa na umahiri wa hali ya juu wa mada ndogo ya *Usanifishaji wa Lugha ya Kiswahili*. Hivyo, kueleza kwa usahihi hatua zote tano zilizofanywa na serikali ya Waingereza katika usanifishaji wa lugha ya Kiswahili kama vile kuteua lahaja ya kiunguja,


kuunda kamati ya usanifishaji, kukubaliana kuhusu mfumo wa sarufi utakaotumika, kutayarisha kamusi na vitabu vya sarufi ya lugha husika na kuandaa wataalamu wa watakaoshughulikia shughuli zote za usanifishaji. Vilevile, watahiniwa hao waliandika utangulizi mzuri na hitimisho zuri linaloendana na swali. Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.



07 Usanifishaji ni kitendo cha kuteua lahaja moja kati ya zilizopo nchini na kuifanya marekebisho katika misamiati na kanuni zake lugha ili itumike na watumiaji wake. Usanifishaji huusisha kusawazisha matamshi na maandishi ya lugha. lugha ya kiswahili ilisanifiwa mwaka 1930 chini ya kamati ya lugha ya Intertemitorial swahili language committee kutoka katika lahaja ya kiunguja. Usanifishaji wa kiswahili ulifanyika chini ya utawala wa mwingereza kipindi cha Gavana Donald Cameroon na wataalamu wali okuwepo ni kama Carl Meinof. wakati wa kusanifisha lugha wataalamu walipitia hatua tano za usanifishaji na zifuatazo ni hatua za usanifishaji wa lugha ya kiswahili.

Uteuzi wa lahaja. mnamo mwaka 1905 mkutano ulifanyika Dar es salaam juu ya suala la usanifishaji na baada ya mkutano huo serikali ya uingereza ilifanya mchakato wa uteuzi wa lahaja ya kusanifisha kuwa msingi wa kiswahili sanifu kutokana na uwepo wa lahaja nyingi za kiswahili hasa katika maeneo ya pwani ya Afrika mashariki. kwa mfano mkutano wa uteuzi wa lahaja ulifanyika mwaka 1928 Mombasa na lahaja ya kimvita, kiamu na kiunguja zilipendekezwa lakini lahaja ya kiunguja ilichaguliwa kuwa msingi wa kiswahili sanifu kwani tayari ilikuwa

07 na machapisho ya kudosha. ili kuwa na enco
para kinadumisi na pia ili kuwa na misa
miati mingi hivyo kiunguja kiliteuliwa
ili kusanifiwa kuwa msingi wa kiswahili
li sanifu.
Kuunda kamati ya usanifishaji baada
ya uteuzi wa lahaja hatua iliyofuata
katika mchakato wa usanifishaji ni
kuundwa kwa kamati ya usanifishaji am
bayo itasimamia na kuratibu shughuli
zote za usanifishaji wa kiswahili. kwa
mfano mwaka 1930 ulifuata mkutano
wa tatu uliofanyika Dar es salaam
ambapo waliunda kamati ya usanif-
shaji ijulikanayo kama Interterritorial
kiswahili language committee. kamati hii
iliratibu shughuli nzima ya usanifishaji
wa kiswahili na mwaka 1930 kiunguja
kilisanifiwa na kuwa lugha sanifu. pia
kamati iliratibu shughuli zote za usan
basaji wa lugha ya kiswahili baada
ya usanifishaji.
Kukubaliana muundo wa sarufi utak
aotumika pia baada ya kuundwa kwa
kamati ya lugha ya mwaka 1930,
wataalamu walijadili kuhusu mfumo
wa sarufi utakaotumika kusanifish
a lahaja ya kiunguja kuwa msingi
wa kiswahili sanifu. wataalamu wali
kubaliana na kusanifisha lugha kwa
kufuata msingi ya sarufi ya lugha
ya kiingereza ambapo waliweza ku-


07 kushughulikia vipengele vyote vya kisarufi. kwa mfano sarufi matamshi kama
Fonolojia, sarufi maumbo kama mofolojia
sarufi maana kama semantiki na sarufi
miundo kama sintaksia. hivyo walifanikiwa
kuandaa mfumo wa sarufi wa kutumia katika kiswahili sanifu.
Kuandaa machapisho, pia hatua iliyofuata katika usanifishaji wa lugha ya
kiswahili ni kutoa machapisho kwa
ajili ya kuhakikisha kuwa wanaeneza
Kiswahili sanifu sehemu mbalimbali nchini
Tanzania kabla ya uhuru. ambapo wali
andaa magazeti mbalimbali, vitabu vya
Kiswahili na majarida ambayo yalikuw
a na maudhui ya kiswahili. pia kulik
uwa na waandishi wa kamusi mbalimbali
na kutafsiri waandishi kwa lugha
ya kiswahili. kwa mfano magazeti yali
yoandikwa yalikuwa kama Habari za
Pwani na Bara, Mamboleo, majarida kama
Mulika na Historia ya kiswahili jarida
la kuandaa hivyo hii ilisaidia katika
kusambaza lugha ya kiswahili sanifu
maeneo mengi sana.
Kuandaa wataalamu, hii ni hatua ya
mwisho iliyofanyika wakati wa usanifi
shaji wa lugha ya kiswahili chini
ya utawala wa waingereza. waingereza
walioandaa wataalamu ambao wali
shughulikia mchakato mzima wa
kusanifisha lugha ya kiswahili

**Kielelezo Na. 7.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 7

Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza vizuri hatua tano za usanifishaji zilizofanywa na serikali ya Waingereza katika kusanifisha lugha ya Kiswahili na kupata alama za juu.

Aidha, asilimia 14.05 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kueleza kwa usahihi baadhi ya hatua za usanifishaji wa lugha ya Kiswahili zilizofanywa na serikali ya Waingereza na kushindwa kueleza hatua nyingine. Aidha, watahiniwa wengine walibainisha hatua

sahihi kama vile; *kuteuliwa kwa lahaja ya usanifishaji*, *kuundwa kwa kamati ya usanifishaji* na *Kuundwa kwa kamati ya sarufi*, japo maelezo yaliyotolewa hayakujitosheleza. Watahiniwa wengine walielezea hatua ya *kuundwa kwa vyombo mbalimbali vya habari kama vile magazeti na redio* ambavyo vilichangia katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru na havikuhusika na usanifishaji wa Kiswahili, hivyo kupata alama za wastani.


Hata hivyo, watahiniwa wachache sawa na asilimia 1.85 ya waliojibu swali hili, walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa uelewa wa mada ndogo ya *Usanifishaji wa Lugha ya Kiswahili*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza hatua zisizo sahihi kama vile; *kuitisha mkutano wa viongozi wa nchi za Afrika Mashariki* ambalo ni moja ya matukio ya usanifishaji na si miongoni mwa hatua za usanifishaji wa Kiswahili. Kutokana na kukosa umahiri huo, watahiniwa wengine walielezea *uanzishwaji wa shule mbambali zinazofundisha lugha ya Kiswahili*, *kuundwa kwa taasisi ya Kiswahili (TUKI)* na *kuundwa kwa vyombo vya habari* ambavyo kiuhalisia ni mchango wa serikali ya Tanzania katika kukuza na kueneza Kiswahili baada ya uhuru lakini havihusiani na hatua zilizofanywa na serikali ya Waingereza katika usanifishaji wa lugha ya Kiswahili, hivyo kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali na kupata alama 0.

7. Usanifishaji; Ni kulinganisha lugha na kuifanya ikubalike miongoni mwa watu wanaohusika kimatumizi. Katika zoezi zima la usanifishaji, kuliweza kuteuliwa kwa lahaja itakayohusika katika shughuli nzima ya usanifishaji ambayo lahaja hiyo ilikuwa ni ung-lahaja ya Kiunguja, lakini baadae kukaja kwa kusanifishwa kwa lugha ya Kiswahili. Zifuatazo ni hatua zilizofanya serikali ya waingereza katika usanifishaji wa lugha ya Kiswahili. hatua hizo ni kama:-

Kuteuliwa kwa lugha ya Kiswahili miongoni mwa lugha nyingine; Hatua ilikuwa ni hatua ya kwanza ambayo ilitumiwa na waingereza katika kuchagua Kiswahili kuwa katika shughuli ya usanifishaji, Kiswahili ili kuteuliwa kulikuwa na sifa zilizokifanya kiteuliwe, sifa hizo ni kuwa na wingi wa watu, ilikuwa inaeleweka katika lugha nyingine.

Kukubaliana na watumizi wa lugha ya Kiswahili; Hatua hii ilikuwa ya pili ambapo baada ya kuteuliwa na kuchaguliwa miongoni mwa lugha nyingine, ilibidi waingereza kuongea na wenyeji watumizi wa lugha hiyo ili waweze kukubaliwa na kuruhusiwa Kiswahili kitumike katika usanifishaji wa lugha.

Kiswahili kuelezwa katika vitabu mbalimbali Kiswahili kilichunguzwa misamiati wake katika vitabu vya sarufi mbalimbali, na kamusi, kwa lengo la kukitafiti Kiswahili kupimwa na kuchunguzwa misamiati yake


Kutumika katika shughuli mbalimbali
hivyo, ikapelekea Kiswahili kukua na
7 kufa kutumika katika usanifishaji.
Kiswahili kutumika katika misuwa
la tofauti nchini; baada ya hatua ya tatu
Kiswahili kuchunguzwa misamiati yake
kiliweza kutumika katika misuwalo mbalimb-
ali nchini kama serikalini, uandishi na
uchapishaji wa vitabu na magazeti
mbalimbali, elimu, katika kufundishia.
Kuteuliwa rasmi kwa Kiswahili
kutumika katika shughuli zote nchini
hii ilikuwa ni hatua ya mwisho
ambapo Kiswahili kiliteuliwa rasmi kuwa
ni lugha ambayo itatumika katika shughuli
zote nchini za kiuchumi, kisiasa na kijamii
pia, itumike katika mawasiliano ya kila
siku kama biashara, kilimo.
Hivyo basi, hizo ndizo hatua kadhaa
zilizotumika na waingereza katika kukifanya
na kukiteua Kiswahili kutumika katika
shughuli nzima ya usanifishaji, kutokana
na hayo, zilizo kuwepo sababu nyingi tu
zilizo kifanya kiteuliwe kama nilivyoeleza
hapo mwanzo kuwa, kilikuwa kimeenea katika
sehemu nyingi nchini, kilikuwa kishatumika
katika maeneo mengi kama elimu n.k.

**Kielelezo Na. 7.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 7


Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili kutokana na kueleza sababu zinazochangia lugha ya Kiswahili kuteuliwa na kuwa lugha rasmi badala ya hatua zilizofanywa na serikali ya Waingereza katika usanifishaji wa lugha ya Kiswahili. Pia, aliandika utangulizi na hitimisho lisiloendana na swali.

### 2.1.2.4 Swali la 8: Utumizi wa Lugha

Swali lilihusu mada ya *Utumizi wa Lugha*, mada ndogo ya *Makosa katika Matumizi ya Lugha* na lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu

vyanzo vya utata katika mawasiliano. Swali lilimtaka mtahiniwa kwa kutumia hoja sita kueleza sababu za watumiaji wa lugha kutomudu kanuni za lugha sanifu.

Takwimu zinaonesha kuwa swali hili lilifanywa na watahiniwa wachache (6,446) sawa na 15.8 kwa kuwa lilikuwa la kuchagua. Miongoni mwao, watahiniwa 2,440 sawa na asilimia 37.85 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 12 hadi 20. Chati Na. 8 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kiasilimia katika Swali la 8.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 8*

Katika Chati Na. 10, watahiniwa 636 sawa na asilimia 9.87 walikuwa na ufaulu mzuri kuanzia alama 12 hadi 20, watahiniwa 1,804 sawa na asilimia 27.98 walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5, na watahiniwa 4,006 sawa na asilimia 62.15 walifaulu kwa kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5.

Takwimu za ufaulu zinaonesha kuwa, zaidi ya nusu ya watahiniwa yaani asilimia 62.15 waliojibu swali hili, walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Utumizi wa Lugha* na mada ndogo ya *Makosa katika Matumizi ya Lugha*. Hivyo, kushindwa kueleza kwa usahihi sababu za watumiaji wa lugha kutomudu kanuni za lugha sanifu. Miongoni mwao, asilimia 3.13 walipata 0. Watahiniwa hao walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu sababu za watumiaji wa lugha kutomudu kanuni za lugha

sanifu kama vile athari za lugha mama, ujumuishaji wa kanuni zinazotawala maumbo ya maneno/miundo ya tungo, ujuzi wa lugha zaidi ya moja, athari za vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, athari za kimaumbile, hisia au huzuni ya mzungumzaji na kiwango cha elimu cha mtumiaji wa lugha. Kutokana na kukosa umahiri huo, baadhi yao walibainisha makosa yanayojitokeza kwa watumiaji wa lugha kama vile *kutumia maneno yenye maana zaidi ya moja*, *kutumia kauli ya utendea*, *kutozingatia mantiki* na *matumizi ya herufi yasiyo sahihi*. Watahiniwa wengine walieleza changamoto za kukua na kuenea kwa Kiswahili kama vile; *uhaba wa wataalamu*, *mfumo wa elimu*, *uhaba wa vitabu*, *kasumba* na *ukosefu wa ajira na fedha* kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mtahiniwa katika swali hili.

| | | |
|---|---|---|
| 08 | Lugha sanifu; Ni lugha iliyosanifu kimaana, kimuundo na kimatamshi. Zipo sababu mbalimbali zinazo wafanya watumiaji wa lugha kutomudu kanuni za lugha sanifu kama ifuatavyo. | |
| | Kutozingatia mazingira; Mara nyingi watumiaji wa lugha hushindwa kumudu kanuni za lugha sanifu kwasababu ya kushindwa kuzingatia maadhari wanapokuwa wakizungumza. Mfano mtu kuzungumza bila kuangalia je yuko kanisani, shuleni, msikitini mtaani au mahakamani. Mfano mtu anaweza kuwa kanisani akamsalimia mchungaji shkamoo mwalimu wakati sio sehemu sahihi ya kusalimia kuhusu mwalimu. | |
| | Kutozingatia uhusiano wa wazungumzaji; Watumiaji wa lugha hushindwa kumudu kanuni za lugha sanifu kwani hushindwa kufahamu ni nani anaongea nae. Mfano yaweza kuwa ni mwalimu na mwanafunzi alafu mwanafunzi akamwambia vipi mshkaji badala ya shkamoo mwalimu hapo kanuni za lugha sanifu zinakuwa zimevunjwa kwani maneno kama hayo ya mshikaji hutumiwa na watu wa rika sawa. | |

n.8 Kutozingatia mada inayohusika; Endapo mtu hatofahamu mada inayozungumzwa miongoni mwa wazungumzaji atakuwa amevunja kanuni za lugha sanifu kwani ili kumudu kanuni za lugha sanifu lazima uzingatie mada ya mazungumzo. Mfano mwalimu yaweza kuwa anafundisha kuhusu mada ya utungaji alafu mwanafunzi anauliza swali kuhusu mada ya tafsiri na ukalimani badala ya kuuliza swali linaloendana na ~~topiki~~ mada ya utungaji

Kutozingatia lengo la mazungumzo; Lengo la mazungumzo linatakiwa kuzingatiwa ili kumudu kanuni za lugha ~~la~~ sanifu lakini watumiaji wa lugha mara nyingi hushindwa kumudu kanuni za lugha sanifu kwasababu ya kutozingatia lengo la mazungumzo. Mfano kama mazungumzo yanalenga kuburudisha, kuonya au kuelimisha mtumiaji wa lugha anatakiwa kufahamu lengo hilo.

Kutozingatia njia bora ya mawasiliano; Ili mtumiaji wa lugha aweze kumudu kanuni za lugha sanifu lazima afahamu ni njia ipi ya mawasiliano atakayotumia kuwasiliana na mwenzake. Mfano, njia ya simu, barua au kuzungumza ana kwa ana. Hivyo sababu kubwa ya watu kutomudu kanuni za lugha sanifu ni kwamba wanashindwa kuzingatia njia ya mawasiliano.

**Kielelezo Na. 8.1**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Katika Swali la 8

Katika Kielelezo Na. 8.1, mtahiniwa alielezea mambo mbalimbali ya kuzingatia katika uteuzi wa lugha ya mazungumzo kinyume na matakwa

ya swali badala ya kueleza sababu za watumiaji wa lugha kutomudu kanuni za lugha sanifu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache asilimia 9.87 waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha juu kuanzia alama 12 hadi 20. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuonesha kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Utumizi wa Lugha* hususani mada ndogo ya *Makosa katika Matumizi ya Lugha*. Watahiniwa hao walimudu kueleza baadhi ya sababu za watumiaji wa lugha kutomudu kanuni za lugha sanifu kama vile athari za lugha mama, ujumuishaji wa kanuni zinazotawala maumbo ya maneno/miundo ya tungo, ujuzi wa lugha zaidi ya moja, athari za vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, athari za kimaumbile, hisia au huzuni ya mzungumzaji na kiwango cha elimu cha mtumiaji wa lugha.


Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alipata alama za juu 17.5 kutokana na kueleza sababu zifuatazo: *athari za lugha mama*, *kutokujua lugha kwa mawanda mapana*, *ukosefu wa msamiati* na *kasumba kwa wasomi*. Majibu ya mtahiniwa huyu yalionekana kuwa na mapungufu kidogo kwani hoja ya kuongeza vitamkwa haikuwa sababu sahihi inayowafanya watumiaji wa lugha kutomudu kanuni za lugha sanifu bali ni makosa yanayojitokeza watumiaji wa lugha wanapokiuka kanuni za lugha sanifu, hivyo kupata alama pungufu. Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Kutomudu kanuni za lugha; Ni
ukosefu wa kufuata sheria na taratibu zilizopo
Q8. katika lugha husika, ukosefu huu hufanywa
na watumiaji wa lugha husika na kusababisha
makosa katika lugha kwa mfano, makosa
ya kisarufi, makosa ya kimuundo, kimatamshi
na makosa ya kimaana. Makosa haya
katika lugha husababisha ukosefu wa
umahiri wa lugha, na hukwamisha kukua
na kuenea kwa lugha husika katika jamii
kwa mfano, watanzania wanaotumia lugha
ya kiswahili hudumaza lugha kwa kutokuzing-
atia kanuni za lugha ya kiswahili. Zifuatazo
ni sababu za watumiaji wa lugha kutomudu
kanuni za lugha sanifu.

Ukosefu wa elimu; kwa mfano;
Watanzania wanaotumia kiswahili hasusani
wanaoishi kijijini wanakosa wajuzi maalumu
wa lugha kwa mfano, waalimu wa lugha
ya kiswahili wa kutosha, hivyo hupelekea
watumiaji wa lugha kukosa elimu au maarifa
yanayohusu lugha husika hivyo basi, ili
kutatua changamoto hii serikali ilenge kuhi-
misha wanajamii hasa kwa kuhamasisha
watu kusomea ualimu wa kiswahili ili kueneza
elimu kwa wengine.

Athari za lugha mama; kwa
mfano; lugha za kikabila nchini Tanzania,
husababisha makosa ya kutokuzingatia
kanuni za lugha ikiwemo matamshi sahihi
ya maneno kwa mfano;
Nkunja husema - Tunatura badala ya kuna-

kula. pia mpare husema "thamani" badala
ya "samani" na mmakonde husema "ntoto"
08 badala ya "mtoto" athari hizi za lugha
mama hujenga mazoea kwa wazungumzaji
wa lugha. hivyo ili kuepuka athari hizi za
lugha mama, wakimbizi wa lugha ya kiswahili
wanapaswa kuzingatia kanuni na sarufi ya
lugha ya kiswahili.
Athari za kimaumbile; kwa mfano,
kilembe wakimbizi wa lugha ya kiswahili
wanashindwa kumudu za kuzingatia kanuni
za lugha sanifu kutokana na athari au
matatizo ya kimaumbile haba kabisa
matamshi ya maneno ya kiswahili. kwa
mfano, mtu mwenye kilembe husema, athari
badala ya "asante" au "thawa badala ya sawa"
ili kuwasaidia wakimbizi wa lugha wenye
matatizo ya kimaumbile, wanapaswa kuelewa
na wajuzi wa lugha ya kiswahili.
Athari za lugha za kigeni; kwa
mfano, kiingereza huleta athari katika lugha
ya kiswahili. hii hutokana na kuwa na
umahiri wa lugha zaidi ya moja, na
kutokuzingatia sarufi ya lugha hiyo hupelekea
athari kusababisha za kuchanganya msamiati
baina ya lugha, kwa mfano, mzungumzaji
wa lugha ya kiswahili husema "nakulove
sana" badala ya "nakupenda sana" au
"ntakuwait nje" badala ya "ntakusubiria
nje" ili kutatua changamoto hii kwa
wakimbizi wa lugha wanapaswa kuelimishwa-
wa na kuelimishwa wanapotumia lugha



Kutokufahamu sarufi ya lugha;
08. kwa mfano; watumiaji wengi wa lugha
ya Kiswahili hawazingatii na kuvunja
kanuni za lugha kwa sababu ya
kutokufahamu sarufi ya lugha ya Kiswahili
inayohusu kanuni, sheria na taratibu
za lugha ya Kiswahili kwa mfano, sarufi
hukusisha, uhomiyi wa lugha, na lingo
mbalimbali za Kiswahili pia matamshi,
maombo na maana za msamiati mbali-
mbali ya Kiswahili.
Kasumba za wasomi; kwa mfano,
wasomi wengi hasa wanaoishi katika
nchi za kigeni, wenye asili ya Tanzania
wanashindwa kumudu kanuni za lugha
sanifu kwani wanadharau lugha ya
Kiswahili na kuiona kama lugha duni
au lugha ya watu wa tabaka la chini
na kukosa uzalendo wa kujivunia
lugha ya Kiswahili.
Kwa kuhitimisha; lugha ina
umuhimu sana katika jamii, ikiwemo
kufanikisha mawasiliano, lugha hukuza
na kutambulisha utamaduni, pia lugha
hutumika kama chombo cha kuleta umoja
na kuunganisha wanajamii, lugha hutumika
katika kazi za fasihi kwa mfano;
riwaya, tamthiliya na mashairi. Kwa
lengo la kuelimisha, kuonya jamii,
kuburudisha jamii, kukosoa wanajamii
na kufichua maovu yanayotendeka
katika jamii.

**Kielelezo Na. 8.2**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 8

Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kwa usahihi sababu za watumiaji wa lugha kutomudu kanuni za lugha sanifu. Mtahiniwa huyu aliandika utangulizi mzuri lakini katika hitimisho alitoa maelezo yasiyojitosheleza, hivyo kutopata alama zote za swali hili.

Hata hivyo, asilimia 27.98 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 7 hadi 12. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kueleza kwa usahihi baadhi ya sababu za watumiaji wa lugha kushindwa kumudu kanuni za lugha sanifu na kushindwa kueleza kwa usahihi sababu nyingine. Miongoni mwao, wapo walioeleza sababu sahihi lakini wakatoa maelezo yasiyojitosheleza na wengine walielezea

hoja chache zilizo sahihi na nyingine zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea hoja ya *uwepo wa utata katika maneno* ambayo inahusiana na neno kuwa na maana zaidi ya moja. Pia, mtahiniwa mwingine alieleza sababu ya *uunganishaji wa maneno* ambayo ni njia ya uundaji wa maneno. Majibu ya watahiniwa hao hayakudhihirisha sababu za watumiaji wa lugha kushindwa kumudu kanuni za lugha sanifu, hivyo kupata alama za wastani.

## 2.2 SEHEMU YA II: KISWAHILI KARATASI YA PILI

Karatasi ya pili imegawanyika katika sehemu A na B. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulikuwa kama ifuatavyo:


### 2.2.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) yenye jumla ya alama 40, ambapo kila swali lilikuwa na alama 10. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii.

#### 2.2.1.1 Swali la 1: Maendeleo ya Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Fasihi Simulizi*, mada ndogo ya *Uhifadhi wa Kazi za Fasihi Simulizi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kwa kutumia hoja tano kutathmini kauli, "Maendeleo ya sayansi na teknolojia yameifanya fasihi simulizi kupoteza uhalisia katika uwasilishaji wake".

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote (40,686) sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani huu. Ufaulu wa watahiniwa ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 22,143 sawa na asilimia 54.42 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na. 9 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Katika Chati Na. 9, watahiniwa 9,665 sawa na asilimia 23.75 walikuwa na ufaulu wa juu kuanzia alama 6 hadi 10, watahiniwa 12,478 sawa na

asilimia 30.67 walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5, na watahiniwa 18,543 sawa na asilimia 45.58 walifaulu kwa kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 3.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa asilimia 23.75 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu walifaulu kwa kiwango cha juu kuanzia alama 6 hadi 10. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Maendeleo ya Fasihi Simulizi* hususani mada ndogo ya *Uhifadhi wa kazi za Fasihi Simulizi*. Watahiniwa hao walifafanua kwa usahihi kauli, "*Maendeleo ya sayansi na teknolojia yameifanya fasihi simulizi kupoteza uhalisia katika uwasilishaji wake*", na kutoa mifano sahihi kuthibitisha hoja hizo. Watahiniwa walitoa hoja sahihi kama vile; *kukosekana kwa ushirikishwaji baina ya fanani na hadhira* kamavile, radio na simu huwasilishwa kwa njia ya sauti; *fanani kukosa uwezo wa kubadilika kulingana na hadhira na mazingira anayokutana nayo* kwa mfano, michezo ya kuigiza kwenye televisheni fanani hawezi kubadilika hata kama watazamaji watakasirika kwani hawaoni; *kutobadilika kwa fasihi simulizi kulingana na mabadiliko ya nyakati na maendeleo ya jamii husika* kwa mfano, hadithi zilizorekodiwa kwenye kanda za sauti na video haziwezi kupokea mabadiliko*; kukosekana kwa utendaji wa hadhira na fanani kutokana na fanani na hadhira kutokuonana ana kwa ana* kwa mfano, hadithi zinazosimuliwa kwenye vipindi vya redio; na *kubadilisha uhalisia wa muonekano wa fanani na hadhira* kwa mfano, vifaa na mifumo ya kiteknolojia hubadilisha sauti au rangi ya fanani na hadhira. Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.


Fasihi simulizi; Ni aina ya fasihi ambayo huwasilishwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo. Njia hii ni kongwe lakini ndio njia ambayo husaidia fasihi kusambaa kwa haraka. Lakini kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia imesababisha kupotea uhalisia. Zifuatazo ni sababu

Kukosekana kwa utendaji; kutokana na baadhi ya kazi kuhifadhiwa katika vifaa mfano vinasa sauti, maandishi; imesababisha fasihi simulizi kukosa utendaji wakati wa uwasilishaji.

Mfano

kupiga makofi,

kutopokea mabadiliko; kutokana na kukua na maendeleo hayo imepelekea kazi ya fasihi kutopokea mabadiliko kwani kuna baadhi ya kazi huhifadhiwa katika vinasa sauti na wakati wa uwasilishaji hapakuwepo na mbinu

Fanani na hadhira hawaonani ana kwa ana; kutokana na maendeleo hayo pia hupelekea fanani na hadhira kutoweza kuonana ana kwa ana kutokana na uhifadhi wake ilipohifadhiwa mfano; katika maandishi.

Inakosa vionjo; Hii kama kazi hii itahifadhiwa katika njia ya sayansi fanani atakosa kuonesha vionjo kama vile kupiga makofi, kutikisa mabega

**Kielelezo Na. 9.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi Katika Swali la 1


Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa hoja sahihi na mifano ili kutathmini kauli inayosema, "*Maendeleo ya sayansi na teknolojia yameifanya fasihi simulizi kupoteza uhalisia katika uwasilishaji wake*".

Aidha, asilimia 30.67 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5. Ufaulu huu ulitokana na

watahiniwa hao kutoa baadhi ya hoja sahihi na nyingine zisizo sahihi. Miongoni mwao, wapo waliotoa hoja sahihi na mifano sahihi kutathmini kauli inayosema, “Maendeleo ya sayansi na teknolojia yameifanya fasihi simulizi kupoteza uhalisia katika uwasilishaji wake” kama vile; *kutokupokea mabadiliko ya papo kwa papo*; *fanani na hadhira kutokuonana ana kwa ana* na hoja nyingine zisizojitosheleza. Hata hivyo, baadhi ya hoja zilikosa mifano na kuwa na maelezo yasiyojitosheleza. Aidha, watahiniwa wengine walitoa hoja zisizo sahihi kama vile; *sayansi na teknolojia imekuwa ya kibiashara, wasanii wa kiafrika kujikana nafsi zao na fanani kupoteza hisia zake kwa hadhira*. Majibu yasiyo sahihi yamesababisha kupata alama za wastani.

Hata hivyo, asilimia 45.58 ya watahiniwa waliofanya swali hili, walitoa majibu yasiyo sahihi na kuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa maarifa ya kutosha juu ya mada ya mada ndogo *ya Uhifadhi wa Fasihi Simulizi* na *Athari za Sayansi na Teknolojia katika Uhifadhi wa Kazi za Fasihi Simulizi*. Baadhi yao, walitoa hoja zinazohusiana na sifa za fasihi simulizi kama vile *ukongwe, uwasilishaji wa mdomo, umiliki wake* na *upokeaji wa mabadiliko* bila kuonesha namna uhalisia wa sifa hizo ulivyoathiriwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Watahiniwa wengine walibainisha njia zote za uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi badala ya kutathmini namna maendeleo ya sayansi na teknolojia yalivyoifanya fasihi simulizi kupoteza uhalisia katika uwasilishaji wake kama vile kukosekana kwa ushirikishwaji baina ya fanani na hadhira; fanani kukosa uwezo wa kubadilika; fasihi simulizi kutopokea mabadiliko ya nyakati; kukosekana kwa utendaji wa hadhira na fanani; na kubadilisha uhalisia wa muonekano wa fanani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza dhima za fasihi kama vile; *kuburudisha jamii*, *kuonya na kuadabisha jamii*, *kuikomboa jamii*, *kukuza utamaduni* na *kuelimisha jamii*; kinyume kabisa na matakwa ya swali hili. Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili kwa kushindwa kukidhi matakwa ya swali.


01. (i) fasihi simulizi ni nyepesi kusahaulika; kwa sababu yenyewe huweza kuwasilishwa kwa njia ya mdomo mfano mtu akifa.

(ii) Fasihi simulizi ni nyepesi kubadilika kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine; hii ni tofauti na uwasilishaji wa njia ya Maandishi au sauti. Mfano Unakuta waliosimuliwa washasahau baadhi ya matukio

(iii) Fasihi simulizi uwasilishaji wake ni wa njia ya mdomo ambapo kuwapata watu ambao wanajua matukio mameshafariki hivyo huwezi kupata taarifa. tofauti na uwasilishaji kwa njia ya maandishi.

(iv) fasihi simulizi ni mali ya jamii nzima; wakati uwasilishaji wa fasihi ya Maandishi sio ya jamii ambayo haiwezi kubadilika Mfano vitabu

(v) fasihi simulizi inahitaji watu wawili ambao ni fanani na hadhira; wakati fasihi andishi ni ya mtu binafsi.

**Kielelezo Na. 9.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Katika Swali la 1


Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza sifa za fasihi simulizi katika hoja ya (i), (ii), na (iv), hoja ya (iii) ni njia ya uhifadhi wa fasihi simulizi na hoja ya (v) ni chanzo na kikomo cha fasihi simulizi, hivyo kupata 0.

### 2.2.1.2 Swali la 2: Fasihi kwa Ujumla

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi kwa Ujumla*, mada ndogo ya *Nadharia ya Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Swali lilipima uelewa wa mtahiniwa katika kuchambua nadharia za kifasihi; na lilimtaka mtahiniwa kufafanua kauli, "*Mhakiki ni msanii aliyebobea katika nadharia, misingi, na utendaji wa taaluma ya utunzi.*"

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote (40,688) sawa na asilimia 100 ya wote waliofanya mtihani. Swali hili lilijibiwa kwa kiwango cha wastani ambapo, watahiniwa 19,367 sawa na asilimia 47.60 walifaulu kwa

kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na. 10 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 10**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 2*

Katika Chati Na. 10, watahiniwa 12,604 sawa na asilimia 30.98 walikuwa na ufaulu wa juu kuanzia alama 6 hadi 10. Watahiniwa 6,763 sawa na asilimia 16.62 walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5, na watahiniwa 21,321 sawa na asilimia 52.40 walifaulu kwa kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 3.

Asilimia 30.98 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu walikuwa na ufaulu mzuri kuanzia alama 6 hadi 10. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Fasihi kwa Ujumla* na mada ndogo ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Watahiniwa hao walifafanua kwa usahihi kauli inayosema, "*Mhakiki ni msanii aliyebobea katika nadharia, misingi, na utendaji wa taaluma ya utunzi*", kwa kutoa hoja tano kama vile; Mhakiki anatakiwa ajue historia na mazingira yaliyomkuza mwandishi; kuelewa historia na siasa ya jamii inayomuhusu; kusoma kazi mbalimbali za fasihi na si hiyo tu anayotaka kuichambua; kuwa na ujuzi wa hali ya juu kuweza kujua kwa kina nadharia ya uchambuzi; asimame katika ukweli wa kazi ya mwandishi bila upendeleo; asiongozwe na hisia zake; na asome tahakiki za wahakiki wengine ili kujiongezea ujuzi. Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kukidhi matakwa ya swali.

Q2. i) Mhakiki anapaswa awe anasoma tahakiki
za wahakiki wengine wa kazi za fasihi;
Sifa ya mhakiki anapaswa asome tahakiki
mbalimbali za wahakiki wengine ili aweze
kupata maarifa mapya kutoka kwa wahaki
ki hao.

ii) Anapaswa afahamu nadharia na misingi
ya kazi za fasihi.
Ili mhakiki akamilike anapaswa misingi miku
uu ya fasihi pamoja na nadharia zake
ili aweze kufanikisha kazi yake ya uhakiki.

iii) Awe anasoma tahakiki za kazi za fasihi.
Sifa ya mhakiki ni kusoma tahakiki mba
li mbali za kazi ya fasihi ili aweze kupa
uzoefu wa kuhakiki kazi za watunzi
wengine bila kuwanyonya.

Q2. iv) Awe anafahamu historia ya jamii husika;
Ili mhakiki aweze kufanikiwa katika kazi yake
ni lazi atambue falsafa na historia ya jamii
anayoishughulikia kwa kuzingatia utamadu
ni na mienendo ya jamii husika.

v) Anapaswa hasiendeshwe na hisia zake tu a
napohakiki kazi za fasihi.
Mhakiki bora ni yule asiyeendeshwa na hisia
zake tu katika kuhakika kazi mbalimbali za
fasihi ni lazima hazingatie matakwa ya jamii
yake pamoja na matatizo yanayoikumba.

**Kielelezo Na. 10.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi Swali la 2

Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua kwa usahihi kauli inayosema, "*Mhakiki ni msanii aliyebobea katika nadharia, misingi, na utendaji wa taaluma ya utunzi*" na kutoa hoja sahihi tano zilizomwezesha kupata alama za juu.

Aidha, asilimia 16.62 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kutoa baadhi ya hoja sahihi kufafanua kauli inayosema, "*Mhakiki ni msanii aliyebobea katika nadharia, misingi, na utendaji wa taaluma ya utunzi*" na kushindwa hoja nyingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile: *mhakiki hufahamu utamaduni wa jamii husika; hutambua mabadiliko mbalimbali yanayojitokeza katika jamii anayoifanyia kazi* na *sharti afahamu vipengele vya fani na maudhui katika kazi ya fasihi anayohakiki*. Hata hivyo, ufafanuzi wake haukujitosheleza ipasavyo, hivyo kupata alama za wastani.

Asilimia 52.40 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu kwa kiwango hafifu na kupata alama kuanzia 0 hadi 3. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa umahiri kuhusu mada ndogo ya *Nadharia za Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walitoa hoja zilizohusiana na uteuzi wa vipengele vya fani katika kazi za fasihi kama vile; *uteuzi mzuri wa lugha*, *uteuzi wa wahusika*, *uundaji wa mandhari* na *uchaguzi mzuri wa tukio*; majibu yanayoonesha kuwa watahiniwa hao hawakuelewa matakwa ya swali kwani walichanganya vipengele vya fani na uhakiki wa kazi za fasihi.

Watahiniwa wengine walifafanua hoja zinazohusu umuhimu wa mhakiki kama vile; *mhakiki humsaidia mwandishi kujua makosa yake* na *humsaidia mwandishi kuandika kazi nzuri*; hoja ambazo ni kinyume kabisa na matakwa ya swali hili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua dhima tatu za mhakiki kama vile; *mhakiki hufafanua na kuweka wazi picha mbalimbali zilizotumika katika kazi za kifasihi*, *hueleza na kufafanua mawazo mbalimbali yaliyojadiliwa katika kazi ya kifasihi*; *hufafanua ujumbe na mafunzo yanayopatikana katika kazi za kifasihi*, hoja ambazo zinaelezea vipengele anavyoshughulikia mhakiki wa kazi za fasihi anapochambua fani na maudhui. Kwa ujumla, watahiniwa hao walitakiwa kufafanua sifa za mhakiki ili kuthibitisha kauli inayosema, "*Mhakiki ni msanii aliyebobea katika nadharia, misingi, na utendaji wa taaluma ya utunzi*." Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili na kupata alama za chini.

kuonyesha madhara ya mila potofu katika ja
mii.
Tatu, Mhakiki huonyesha ufundi wa Lug
ha uliotumiwa na Mwanafasihi kupitia
kazi zao kama ushairi. Kwa mfano Diwani
ya KIMBUGA Haji Gora Anasawiri taswira
ya "kimbwagai". Vile Vile Penina Mhando
Anaonyesha Taswira mbali mbali kama vile
"NGUZO YA USWEZI" Akimaanisha Azimio la
Arusha.
Vile Vile. Mhakiki huonyesha falsafa
ya Mwanafasihi au Mtunzi kupitia kazi m
bali mbali za fasihi. Kwa mfano KILIO CHETU
Medical Aid foundation Wanaonyesha mtaza
mo wa Kimapinduzi juu ya umuhimu wa el
imu ya kujitambua kwa kijana, Namna ita
kavyo msaidia kuepukana na Maradhi ya
Kingono.
pia. Mhakiki ni daraja kati ya Mwan
afasihi na Hadhira. kupitia mhakiki had
hira huburudika, huelimika na hata kutun
za Mila na Desturi za jamii husika. Kwa
huyo Mhakiki ni chanzo cha Maendeleo.
Kiujumla, Mhakiki ni Muhimu mno
katika kazi yoyote ya fasihi kwani kupitia
yeye jamii huelimika, huburudika na kueny
a au kuadibu na Hata kutunza mali na jamii
Husika.

**Kielelezo Na. 10.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 2


Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili, kwani alifafanua dhima za mhakiki wa kazi za fasihi badala ya sifa zake kama ilivyotakiwa.

### 2.2.1.3 Swali la 3: Maendeleo ya Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Fasihi Simulizi*, na mada ndogo ya *Tanzu wa Fasihi Simulizi*. Swali lilipima uelewa wa dhana mbalimbali za kifasihi; na lilimtaka mtahiniwa kueleza dhana zifuatazo za kifasihi: (a) Mafumbo, (b) Lakabu, (c) Misemo, (d) Nahau na (e) Mizungu.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote (40,688) sawa na asilimia 100 ya wote waliofanya mtihani. Swali hili lilijibiwa kwa kiwango cha wastani

ambapo, watahiniwa 19,913 sawa na asilimia 48.94 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na. 11 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 3*

Katika Chati Na. 11, watahiniwa 9,396 sawa na asilimia 23.09 walikuwa na ufaulu mzuri kuanzia alama 6 hadi 10, watahiniwa 10,517 sawa na asilimia 25.85 walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5, na watahiniwa 20,775 sawa na asilimia 51.06 walifaulu kwa kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 3.

Watahiniwa waliojibu swali hili (20,775) sawa na asilimia 51.06 hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu dhana anuwai za kifasihi walizopewa hivyo kushindwa kutoa maelezo sahihi ya dhana hizo. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa umahiri katika mada ndogo ya *Tanzu za Fasihi Simulizi*. Baadhi yao walionesha kutokuelewa dhana hizo, hivyo kutoa maelezo yasiyo sahihi ya dhana walizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea dhana hizo kama vile (a) Mafumbo ni *hadithi au maneno yanayohitaji kufumbuliwa ili yalete maana*; (b) Lakabu ni *nyimbo zinazoimbwa sehemu za starehe au huzuni*; (c) Misemo ni *hadithi ambazo husemwa kwa lengo la kufikisha ujumbe fulani kwa mficho*; (d) Nahau ni *maneno yaliyobeba maana zaidi ya moja ili kufikisha ujumbe fulani*; na (e) Mizungu ni *hadithi zinazooneshwa kwa wakati au kipindi maalumu*. Watahiniwa hao walitakiwa kuelezea dhana za kifasihi kama

ifuatavyo: (a) Mafumbo ni *kauli za maneno ya kawaida lakini zinazoficha maana kwa kutumia picha na mafumbo*; (b) Lakabu ni *majina ya kupanga ambayo baadhi ya watu hupewa kutokana na sifa zao za kimwili, kinasaba, kitabia, na kimatendo*; (c) Misemo ni *tungo zinazotumia lugha ya picha, ishara na tamathali kuelezea kitu*; (d) Nahau ni *fungu la maneno lenye maana maalumu isiyotokana na maana ya kawaida za maneno hayo*; na (e) Mizungu ni *kauli zenye picha za mafumbo zinazoonesha ukinzani wa fikra au tukio*. Kielelezo Na.11.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili na kupata 0.


3. Dhana za Kifasihi
a) Mafumbo: ni maneno yanayotumika katika kazi za kifasihi ili kuweza kufikisha ujumbe kwa hadhira.
b) Lakabu: ni mbinu za kifasihi ambayo mwandishi anatumia katika kutafsiri fasihi.
c. Misemo: Ni tanzu za fasihi ~~simulizi~~ ~~ambayo~~ andishi ambayo inatumia misemo kama vile "utatupa roho yako"
d) Nahau: Ni fasihi inayotumia kutafsiri, ~~tamathali~~ thamatali mbalimbali za fasihi andishi kama vile.
Ndio uti wa mgongo mti huo"
e) Mizungi: Ni fasihi inayotumika kufikisha ujumbe kwa wahusika

**Kielelezo Na. 11.1**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Katika Swali la 3

Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza dhima za dhana alizopewa kinyume na matakwa ya swali hili badala ya kueleza maana za dhana anuwai alizopewa na kupata 0.

Aidha, asilimia 25.85 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kueleza kwa usahihi baadhi ya dhana na kushindwa kuelezea dhana nyingine. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alieleza kwa usahihi dhana za vipengele (b) Lakabu ni *majina ya kupanga ambayo*

*hupewa mtu au hujipa mtu mwenyewe kutokana na sifa aliyokuwa nayo*; (d) Nahau ni *kauli fupi fupi ambazo huelezea maana ambayo haipo wazi*; na (e) Mizungu ni *kauli za mafumbo zenye kutumia maneno ya ukinzani ndani yake* na kutoa mifano sahihi kwa dhana hizo. Kwa upande mwingine, mtahiniwa huyo alishindwa kueleza kwa usahihi dhana katika vipengele (a) na (c), hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache sawa na asilimia 23.09 waliojibu swali hili, walikuwa na ufaulu mzuri wa alama kuanzia 6 hadi 10. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuwa na uelewa wa kutosha wa mada ndogo ya *Tanzu za Fasihi Simulizi*. Baadhi yao walieleza kwa usahihi dhana zote tano walizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kwa usahihi dhana hizo kama vile; (a) Mafumbo ni *kauli za maneno ya kawaida lakini zinazoficha maana kwa kutumia picha na mafumbo*; (b) Lakabu ni *majina ya kupanga ambayo baadhi ya watu hupewa kutokana na sifa zao za kimwili, kinasaba, kitabia, na kimatendo*; (c) Misemo ni *tungo zinazotumia lugha ya picha, ishara na tamathali kuelezea kitu/jambo*; (d) Nahau ni *fungu la maneno lenye maana maalumu isiyotokana na maana ya kawaida za maneno hayo*; na (e) Mizungu ni *kauli zenye picha za mafumbo zinazoonesha ukinzani wa fikra au tukio*. Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kukidhi matakwa ya swali.

3 (b) Lakabu

- Ni majina ya kubuni ambayo watu hupewa kulingana na sifa zao zinazoendana na Majina hayo.

Mfano

Baba wa taifa: Julius. K. Nyerere

Mvivu: Mzembe.

Simba: Mfaume kaubwa

3 (a) Mafumbo.

- Ni semi zenye Maana iliyofichika ambazo hutolewa kwa hadhira ili aweze kuifumbua Maana hiyo

Mfano. Anayejenga Nyumba haitumii na huitumia asiyejenga ~~ep~~ Fumbo hili humani sha Maiti na jeneza kwani Maiti huzikwa kwenye jeneza ambalo haijatengeneza....

3. (c) Misemo
Ni fungo fupifupi na aghalabu hutumia picha, tamathali na ishara ili kuelimisha au kuadilisha
- Misemo pia huweza kuonesha Mahali au Mandhari.
- Misemo huanza na ~~kitenzi~~ nomino na kufuatiwa na kitenzi au Maneno Mengine
Mfano – Elimu ni bahari
– Dunia ~~ni~~ haina Mwisho.
N T

3 (d) Nahau
Ni fungu la Maneno lenye Maana maalumu isiyotokana na Maana za kawaida za Maneno hayo.
- Muundo wa nahau huanza na kitenzi kisha hufuatiwa na Nomino
- Nahau pia hodekeza mazingira au Mandhari
Mfano.
Amevaa Miwani
zunguka mbuyu
KT N

3 (e) Mizungu.
Ni kauli za Mafumbo zenye Ukinzani wa fikra au tukio. Mbali na vitendawili vya kawaida kuna vitendawili vingine vinavyolika navyo kama Mizungu
Mfano – embe limeiva nyumbani, ili siwezi kulila.
– Ua zuri sana limeota Mibani lakini siwezi kulichuma.

**Kielelezo Na. 11.2**: Sampuli ya Majibu Sahihi Katika Swali la 3

Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kwa usahihi dhana alizopewa katika vipengele vyote vitano vya swali hili na kupata alama za juu.

### 2.2.1.4 Swali la 4: Usanifu wa Maandishi

Swali lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi* hususani mada ndogo ya *Usanifu wa Maandishi*. Swali lilipima uelewa wa mtahiniwa wa kuchambua matini za kifasihi, na lilimtaka mtahiniwa kusoma matini ifuatayo kisha kubainisha vipengele vya kifani vilivyotumika katika matini hiyo.


> *Bwana Majivuno, Meneja wa Kampuni, mtafuna mali za umma; alijiona kuwa umma umekubali kumpokea. Akaanza kujisifu kuwa, kati ya mameneja wote nchini, yeye ndiye aliyejua shida za wananchi peke yake. Kumbe bwana, "Waswahili wamejawa na busara." Kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa kuwa waswahili husema kuwa, "Adhaniaye amesima aangalie asianguke." Mzee wangu bwana Bubase aliwahi kuniambia kuwa, ukiona mtu haridhiki na cheo chake, ujue huyo ni rahisi kununuliwa na kuisaliti jamii.*
>
> *Huyu ndiye alikuwa bwana Majivuno, ambaye ni paka- shume ofisini kwake, mtaani kigogo na fataki. Nyumbani je? Nyumbani kwa watoto ni simba. "Aungurumapo simba, mcheza nani?" Ha! Haa! ule ucheshi wake wa ofisini haukuonekana kwa mabinti zake kumi na tatu aliokuwa nao. Jamaa alikuwa jemadari kweli asiye na mchezo. Watoto wake walizoea kumuita "Mdingi," wakisikia gari nje, unasikia wanaambizana … Mdingi anaingia …wote hufyatukia vyumbani mwao fyuuuuuuuu!*
>
> *Bwana Majivuno alitoa amri kuwa mabinti zake wote wawe wamerudi nyumbani ifikapo saa kumi kamili jioni, na wasitoke tena. Sasa hapo ndipo nawaungamia tena waswahili kwa kusema kuwa, "Mkuki kwa nguruwe mtamu, kwa binadamu ni shubiri." Alikuwa bonge la "fataki" kwa mabinti wa wenzake huku kwa wa kwake akiwa pilipili. Kila siku asubuhi, watoto wake wote hupita kwa mstari kutoa "shikamoo" …ole wake asiyepita. Anakinukisha asikwambie mtu. Usiku kabla ya kulala hivyo hivyo shikamoo lazima imtembelee bwana huyu; yeye akiwa amekaa kwenye kochi huku akiwa kifua wazi, tumbo nje kama kiroboto.*
>
> *Wakati wa kula, Majivuno alizoea kukohoa; siyo kikohozi cha ugonjwa, bali kikohozi cha kuonesha uzito na mamlaka aliyonayo. Kikohozi hiki kiliwadokeza kuwa huyu ndiye mwenye ukuu na enzi kwenye nyumba hii. Kila alipokohoa mabinti zake sharti waitikie, "Ewaaaa!" …. Ole wako kwa atakayekosa kuitikia.*
>
> *Akiwa nyumbani aliweza kuongea na mke wake tu., labda kwa kuwa waswahili hawakusahau kusema kuwa, "Siri ya mtungi aijuaye*

*kata." Utasikia anaita mke wake "Majivuno" .... Naye huitika "Labeka mke wangu." Pamoja na kuwa aliweza kuongea na mke wake, lakini mara zote ilikuwa ni kutoa amri tu, huku mkewe akifurukuta kwa kuzipangua na kumpa makavu yake.*

*Siku moja mke wake alimwambia, Mume wangu acha kula mali ya umma. Utafungwa!" Majivuno akajibu, "nimekula kuku mzima peke yangu sembuse……. Majivuno hunijui nilivyo simba siguswi, sisogelewi". Lebeka akaendelea kumwambia, "zee zima, cheo kikubwa bado mtaani linaitwa fataki." Majivuna naye akajibu, "mwanaume huachana na matata yake kaburini." Kisha akatoa amri, "Niletee bia haraka!" "Siendi! Na sitaki tabia za kunywa kunywa pombe ovyo! Nakwambia leo hunywi! Umenisahau ee…?*

*Huyu ndiye Majivuno, Meneja wa Kampuni, ofisini paka-shume, mtaani kigogo na fataki, nyumbani kwa watoto simba. Vipi mkewe?*

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 40,686 sawa na asilimia 100 ya wote waliofanya mtihani. Hili ni swali lililojibiwa vizuri sana na idadi kubwa ya watahiniwa ambapo watahiniwa 37,637 (92.51%) walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na. 12 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kiasilimia katika Swali la 4.




**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 4*

Katika Chati Na. 12, watahiniwa 24,962 sawa na asilimia 61.36 walikuwa na ufaulu mzuri kuanzia alama 6 hadi 10, watahiniwa 12,675 sawa na asilimia 31.15 walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 hadi

5.5, na watahiniwa 3,049 sawa na asilimia 7.49 walifaulu kwa kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 3.

Watahiniwa wengi, asilimia 61.36 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa juu kuanzia alama 6 hadi 10. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuwa na umahiri wa kutosha kuhusu mada ndogo ya *Usanifu wa Maandishi*. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuchambua kwa usahihi vipengele vyote sita vya kifani ambavyo ni *muundo, mtindo, wahusika, mandhari, matumizi ya lugha*, na *taswira/picha* katika matini waliyopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha kwa usahihi vipengele hivyo kuwa; muundo ni *wa rejea*; mtindo ni *wa majibizano, muundo wa nafsi na muundo wa masimulizi*; wahusika ni mhusika mkuu *Bwana Majivuno* na wahusika wasaidizi ambao ni *Mke wa Majivuno na Watoto wa Majivuno ambao ni mabinti kumi na tatu*; matumizi ya lugha kama *methali, misemo, tashibiha, tashihisi, takriri na mdokezo*; na mandhari *ya ofisini kwa Majivuno na nyumbani kwake*. Mtahiniwa huyu alibainisha kwa usahihi vipengele vya fani na kutoa mfano sahihi kwa kila kipengele kama vilivyojitokeza kwenye matini aliyopewa. Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.

4. i. Muundo

- Muundo uliotumika ni Muundo rejea au rukia, ambapo unachanganya matukio yaliyopita, yaliyopo na yajayo.

ii. Mtindo

- kuna Mitindo mingi iliyotumika mfano Mtindo wa majibizano katiya Bwana Majivuno na Mkewake, pia Mtindo wa nafsi umetumika kati kai kumweleza Bwana Majivuno

iii. Mandhari

- Mandhari zilizotumika ni tatu yaani nyumbani kwa Bwana majivuno, Ofisini kwa Bwana majivuno pia na Mtaani ambapo watu wakimuita Bwana majivuno kwa fataki

iv. Wahusika


- Bwana majivuno
- Mke wake
- watoto wake

v. Matumizi ya lugha.

⇒ Misemo imetumika mfano Mkuki kwa nguruwe mtamu, kwa binadamu ni shubiri

⇒ Tanakali sauti imetumika Mfano Bwana majivo anapocheka Ha!, Haa! Haaa!

⇒ Tashibiha Mfano Tumbo wake kama kiroboto



c) Misemo; Ni semi zinazotumia lugha ya picha katika kuwasilisha maana pia huacha swali kwa kujibiwa Mfano Mkuki kwa nguruwe? Kwa binadamu mchungu.

d. Nahau; Hizi ni semi pia ambazo hutenga katika kutoa mafunzo yake kwa swali na lugha ya mafumbo Mfano simba mwenda pole? ndiye mla nyama.

e) Mizungu; Hizi ni semi ambazo pia hutumia lugha ya picha Mfano Nyumbani kuna papai limeiva lakini nashindwa kulichuma. ambapo maana yake ni mtu na mdogo wake wa kike


**Kielelezo Na. 12.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 4

Katika Kielelezo Na.12.1, mtahiniwa alibainisha kwa usahihi vipengele vya kifani katika matini ya nathari aliyopewa. Aidha, mtahiniwa huyo alionesha umahiri wa hali ya juu kwani alielezea maana ya kila kipengele husika na namna kilivyotumika katika matini kwa usahihi, hivyo kupata alama za juu.

Aidha, asilimia 31.15 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5. Ufaulu huu ulitokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kuhusu mbinu za kifani zilizotumika katika matini waliyopewa. Watahiniwa hao walichambua kwa usahihi baadhi ya vipengele vya kifani na kushindwa vingine kwa kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya *Usanifu wa Maandishi* na kifungu cha nathari kwa ujumla. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha kwa usahihi baadhi ya vipengele vya fani kama vile; *mtindo wa masimulizi, mandhari ya nyumbani, mtaani na ofisini* na *wahusika* (*Majivuno, Watoto, Mke wa Bwana Majivuno*; lakini alibainisha muundo wa matini hiyo kuwa ni *wa moja kwa moja* badala ya muundo rejea uliotumika katika matini

hiyo. Aidha, mtahiniwa mwingine alibainisha baadhi ya mbinu za kifani zilizo katika matini isivyo. Kwa mfano, alibaini kauli zifuatazo; *Adhaniaye amesimama aangalie asianguke*, *Siri ya mtungi aijuaye kata* na *Mkuki kwa nguruwe mtamu kwa binadamu shubiri* kama misemo badala ya methali, hivyo kupata alama za wastani.

Asilimia 7.49 ya watahiniwa waliojibu swali hili, walifanya vibaya na kuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa uelewa wa kutosha kuhusu mada ya *Usanifu wa Maandishi* na kifungu cha nathari kwa ujumla. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walitaja vipengele vya matumizi ya lugha badala ya vipengele vya fani kama swali lilivyowataka. Hata hivyo, wapo walioorodhesha vipengele hivyo bila kutoa mifano namna vilivyotumika katika matini waliyopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliorodhesha vipengele vifuatavyo: *tamathali za semi*, *misemo*, *nahau*, *methali*, *tashihisi* na *tashibiha* bila maelezo yoyote. Mtahiniwa mwingine alichambua tamathali za semi peke yake kama vile *tashihisi*, *tashtiti*, *tashibiha*, *mdokezo*, *tafsida*, na *mubalagha* ambazo ni mbinu nyingine ya kisanaa katika kipengele cha matumizi ya lugha, hivyo kuwa na alama pungufu. Aidha, watahiniwa wengine walichanganya vipengele vya fani na vya maudhui kwa kubainisha vipengele kama vile *ujumbe*, *dhamira*, na *falsafa* kinyume cha matakwa ya swali. Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili.


4 (i) Nahau.
(ii) Taswira
(iv) Methali
(v) Rejeota
(vi) Mdokezo
(vii) Mshangao.
(viii) Tanakali sauti

**Kielelezo Na. 12.2**: Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 4

Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyebainisha vipengele vya matumizi ya lugha na mbinu nyingine za kisanaa bila kutoa maelezo yoyote. Mtahiniwa alipaswa kuchambua kwa mifano vipengele vya kifani vilivyounda matini aliyopewa ambavyo ni *muundo, mtindo, wahusika, mandhari, matumizi ya lugha*, na *taswira/picha*.


### 2.2.2 SEHEMU B MASWALI YA MAJIBU MAREFU

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) ya insha ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu. Swali la tano lilikuwa la lazima. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 60 na kila swali lilikuwa na alama 20.

#### 2.2.2.1 Swali la 5: Uhakiki wa Ushairi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi*. Swali hili lilikuwa la lazima na lilimtaka mtahiniwa kufafanua rai kuwa, "Jamii ikikosa maadili ni sawa na nyumba iliyojengwa pasipo msingi imara" kwa kutoa hoja nne kwa kila diwani katika diwani mbili alizosoma.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 40,687 sawa na asilimia 100 waliofanya mtihani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo watahiniwa 37,642 sawa na asilimia 92.52 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 7 hadi 20. Chati Na. 13 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia katika swali la 5.




**Chati Na. 13**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Katika Chati Na. 13, watahiniwa 34,939 sawa na asilimia 85.88 walikuwa na ufaulu wa juu kuanzia alama 12 hadi 20, watahiniwa 2,703 sawa na asilimia 6.64 walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5, na watahiniwa 3,045 sawa na asilimia 7.48 walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi (85.88%) waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu mzuri kuanzia alama 12 hadi 20. Miongoni mwao, watahiniwa 16,389 sawa na asilimia 40.28 walikuwa na ufaulu wa juu kwa kupata alama kuanzia 17 hadi 20. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi*. Watahiniwa hao walifafanua kwa usahihi rai kuwa, "Jamii ikikosa maadili ni sawa na nyumba iliyojengwa pasipo msingi imara" kwa kuonesha namna jamii isiyo na maadili inavyoweza kuathirika na mambo mbalimbali kama vile; *usaliti, mifarakano katika ndoa*, *wizi wa mali za umma*, *unyanyasaji wa wanyonge*, *ukahaba*, *uongozi mbaya*, *kutowaheshimu wazazi*, *chuki* na *dhuluma*. Pia, watahiniwa hao waliandika utangulizi mzuri na hitimisho zuri lililoendana na swali, japo walikuwa na mapungufu madogo madogo katika nukuu za mashairi. Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kukidhi matakwa ya swali.

05. Maadili, hii ni mienendo ambayo inaendana sana na mahitaji ya jamii ambayo imeambatana na sifa njema, matendo mema kama vile uhinikiano, adabu, heshima na usafi katika jamii. Maadili ndio huifanya jamii kuwa na watu waliostaarabika na waliostaarabu katika jamii. Kama jamii ikikosa maadili husababisha majanga ndani ya jamii hiyo." Ni kweli kuwa jamii inapokosa maadili ni sawa na nyumba iliyojengwa pasipo msingi imara" kwani nyumba hiyo yaweza kuanguka au hata madhara mengine. Kwa kutumia diwani mbili ambazo ni "FUNGATE YA UHURU" iliyoandikwa na Mohamed S. Khatib pamoja na diwani "KIMBUNGA" iliyoandikwa na Haji Gora, waandishi hawa wanaonesha madhara ya jamii kutokuwa na maadili.

Kwa kuanza na diwani ya Fungate ya Uhuru mwandishi ameweza kuonesha mambo hayo kama ifuatavyo:-

Kuibuka kwa matabaka katika jamii, jamii inapokosa maadili hupelekea kukosekana kwa upendo kati ya tabaka fulani la watu na tabaka lingine hasa tabaka la maskini na matajiri pamoja na tabaka la werevu na wajinga lakini pia tabaka la viongozi na raia. Hii inajidhihirisha katika shairi la "Waja wa Mungu" ambapo mshairi anasema

"Duniani, nguo mbovu matakoni, makafiri,
Lakini, nguo tele kabatini, mabepari,
Abadani hawa si waja wa Mungu"

Mwandishi anaonesha kuwa matajiri ndio hupewa huduma na vitu na pia kuzingatiwa kuliko maskini. Hata katika jamii zetu mara nyingi watu wenye kipato kikubwa ndio huzingatiwa sana katika kupewa huduma kuliko hata maskini.

05. Hupelekea kukosekana kwa mapenzi ya kweli na usaliti, Msanii anaonesha kuwa jamii inapokosa maadili hupelekea kukosekana kwa mapenzi ya dhati baina ya watu wawili au na jamii yake na pia hupelekea kuibuka kwa usaliti ndani ya mahusiano. katika shairi la "Siwowo" mshairi anasema

" Siwowo,
Ulinijia mapema kama ukinda yatima,
nikawa wako kama baba na mama,
Kakulea kwa ugonjwa na uzima."

Hiyo mwandishi anaonesha kuwa japo jamii au watu wanafadhiliwa kwa kukosa maadili lakini wanaamua kuwasaliti watu wao. Hata katika jamii zetu watu wamekuwa wasaliti na hiyo ndoa nyingi na mahusiano yamevunjika miongoni mwa watu.

Kwa kumalizia na diwani ya Kimbunga mwandishi ameonesha madhara hayo yafuatayo :-

Hupelekea kuwepo kwa wizi wa mali za umma, mwandishi anaonesha kuwa jamii inapokosa maadili hupelekea watu fulani kuwa wanyakuaji wa mali za wengine. katika shairi la "Paka ... " mshairi anasema

"Paka nakuwa wizi, wacha kuiba samaki,
Imekuwa yako kazi, majikoni hundoki,
Hamfai Uchokozi, si kizuri kitu hiki,
paka nakuwasa wizi, wacha vitoweo."

Hiyo mwandishi anaonesha kuwa kwa kukosa maadili katika jamii watu huonyesha tabia mbaya za udokozi wa mali za watu katika jamii. Hata katika jamii zetu kumekuwepo na wimbi kubwa la vijana, wazee na watu wazima wanaojihusisha na wizi hiyo inaonesha kuwa jamii zetu zimekosa maadili mema.

**Kielelezo Na. 13.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 5

Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua kwa usahihi rai kuwa *jamii ikikosa maadili ni sawa na nyumba iliyojengwa pasipo msingi imara* katika diwani ya "Fungate ya Uhuru" na kutoa mifano sahihi ya mashairi ili kuthibitisha rai hiyo.

Aidha, asilimia 6.64 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kufafanua kwa usahihi baadhi ya hoja na kushindwa

kufafanua hoja nyingine. Pia, wapo waliotoa hoja sahihi lakini wakatoa ufafanuzi usiojitosheleza kwa baadhi ya hoja zilizotolewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kufafanua rai kuwa, *jamii ikikosa maadili ni sawa na nyumba iliyojengwa pasipo msingi imara*, alitumia diwani ya "Fungate ya Uhuru" kufafanua hoja ya *wizi* kama athari mojawapo ya ukosefu wa maadili lakini nukuu ya ubeti aloutumia ilikosewa hasa mstari alioubainisha. Kadhalika, katika diwani ya "Chungu Tamu" hoja ya *uzurufu*, mistari ya ubeti alionukuu haikueleza uzurufu bali ilihusu mwanamke anayejitunza na kujiheshimu. Mtahiniwa mwingine alielezea hoja ya *umaskini* lakini alishindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza kuwa ni kwa namna gani jamii inapokosa maadili husababisha umasikini. Upungufu uliojitokeza katika majibu hayo uliwafanya watahiniwa hao kupata alama za wastani.

Asilimia 7.48 ya watahiniwa waliojibu swali hili, walijibu vibaya na kuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi*. Watahiniwa wengi katika kundi hili walijadili dhamira mbalimbali zilizojitokeza katika diwani walizosoma bila kuzihusianisha na na athari ya ukosefu wa maadili katika jamii kama swali lilivyotakiwa kujibiwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika diwani ya "Kimbunga" alifafanua ujumbe uliopo katika diwani hiyo kama vile; *umuhimu wa kuwaheshimu wazazi*, *umuhimu wa kuweka akiba*, *mapenzi ya dhati* na *umuhimu wa kutoa shukrani;* majibu ambayo ni kinyume na athari ya ukosefu wa maadili katika jamii. Mtahiniwa mwingine katika diwani ya "Fungate ya Uhuru" alifafanua ujumbe kama vile: *kuwa na mapenzi ya dhati, umuhimu wa umoja na mshikamano, kupiga vita wizi, dhuluma* na *usaliti*. Ufafanuzi wa ujumbe huo unaonesha mafunzo yanayotolewa na mwandishi ili kujenga jamii bora badala ya kufafanua athari za jamii inapokosa maadili. Kielelezo Na. 13.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyo sahihi katika swali hili.


5 Maadili ni mafundisho mema ambayo mtu anayapata kutoka kwa mtu fulani jamii ya kitu fulani. Ni kweli ya kuwa maadili ni sawa na nyumba iliyojengwa pasipo msingi imara kwa hiyo maadili ni msingi imara sana katika jamii ya sasa. Kwa kutumia diwani ya "KIMBUNGA" iliyoandikwa na Haji Gora pamoja na "FUNGATE YA UHURU" iliyo andikwa na Mohamed S. Khatibu. Kudhibitisha maadili yaliyofichwa na wandishi kwa jamii. Kwa kuanza na diwani ya "FUNGATE YA UHURU" mwandishi anaonesha maadili aliyoyafua kuimarisha msingi katika jamii yake.

Kupiga vita uongozi mbaya, jamii ikikosa uongozi mzuri inakuwa sawa na nyumba iliyokosa msingi. Hivyo mwandishi anatupa maadili ya kupiga vita uongozi mbaya. Kwa mfano katika shairi la "Fungate" mwandishi anasema.

"Fungate ya uhuru, Bado inaendelea
Harusi wana nuru, wazazi wakavutia
Wengi wamesusa, na tena wanaununa"!

Hivyo basi jamii yapasawa kupiga vita suala la uongozi mbaya katika jamii ili kuwa na msingi imara.

Kupiga vita wizi, pia katika jamii ya sasa suala la wizi limekuwa ni tatizo kubwa kwa sasa hivyo basi ili kujenga vera msingi mzuri katika jamii yapasa kupiga vita suala la wizi. Kwa mfano mwandishi anatueleza katika shairi la "Wizi" kwa kusema ya kuwa.


5 "Wizi umo
Kani-sani
msikitini
Hekaluni
Wanyang'wanyang'anyao ni waumini"
Hivyo basi ili tujenge msingi ulio imara katika jamii ya sasa yatupasa kujenga na kupiga vita suala la wizi katika jamii ya sasa.
Kupiga vita umasikini, pia waandishi wa diwani wanaendelea kutupatia maadili katika jamii kwa kutuasa kupiga vita umasikini. Kwa mfano katika shairi la "Wingu" mwandishi anasema.
"Wingu
Wingu limetanda
limetanda na kutughabika
gubi"
Hivyo basi waandishi wametupa maadili ya kupiga vita suala la umasikini katika shairi hilo ili tuweze kutengeneza msingi ulio imara katika jamii ya sasa.
Kupiga vita umalaya, pia ili tuwe na msingi ulio bora katika jamii ya sasa waandishi wetu wanatupa mbinu ya kupiga vita suala la umalaya katika jamii kwa mfano katika shairi la "Paka shume" mwandishi anasema.
"Paka mtaka vya watu, Ikukufika ajali
utumbua kama chatu, nyumbani kumbuka
Hutaputa kitu kwani, umeonyewa ni
mkali"


**Kielelezo Na. 13.2**: Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 5

Kielelezo Na. 13.2 kinaonesha sampuli ya sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua hoja zinazoonesha mikakati ya kujenga jamii yenye maadili mema, badala ya kufafanua ukosefu wa maadili unavyoharibu au kubomoa misingi imara ya jamii. Hata hivyo, mtahiniwa, alitoa utangulizi sahihi na kupata alama 1.

#### 2.2.2.2 Swali la 6: Uhakiki wa Ushairi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, na mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kutathmini ukweli wa kauli "Watunzi wa mashairi ni weledi wa kuteua mandhari yenye uwezo wa kufikisha ujumbe kwa jamii husika" kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu katika diwani mbili alizosoma.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 23,873 sawa na asilimia 58.7 ya wote waliofanya mtihani huu. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi ambapo watahiniwa 22,244 sawa na asilimia 97.37 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kuanzia alama 7 hadi 20 kama inavyoonekana katika Chati Na. 14.




**Chati Na. 14**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Chati Na. 14 inaonesha kuwa, watahiniwa 20,822 sawa na asilimia 87.22 walikuwa na ufaulu mzuri kuanzia alama 12 hadi 20, watahiniwa 2,422 sawa na asilimia 10.15 walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5, na watahiniwa 629 sawa na asilimia 2.63 walifaulu kwa kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5.

Takwimu za ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 87.22 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu mzuri kuanzia alama 12 hadi 20. Miongoni mwao, watahiniwa 6,072 sawa na asilimia 25.43 walijibu vizuri zaidi na kupata alama kuanzia 17 hadi 20. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kutathmini kwa usahihi ukweli wa kauli "Watunzi wa mashairi ni weledi wa kuteua mandhari yenye uwezo wa kufikisha ujumbe

kwa jamii husika." Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika diwani ya "Chungu Tamu" alitoa hoja sahihi kama vile; mandhari ya Dar-Es-Salaam yenye ujumbe wa kufanya kazi kwa bidii ili kuondokana na hali ngumu ya maisha (shairi la Manzese mpaka Ostabei); mandhari ya Kagera imeibua ujumbe kuhusu uzalendo (Daktari Askari); mandhari ya nyumbani yenye ujumbe wa usaliti kama chanzo cha migogoro katika jamii (Fikra za Waungwana).

Mtahiniwa mwingine kwa kutumia diwani ya "Kimbunga" alionesha mandhari kama vile; mandhari ya Zanzibar yenye ujumbe wa umuhimu wa malezi bora katika jamii (shairi la Vijana wa Zanzibar); mandhari ya nyumbani yenye ujumbe wa kuwaheshimu wazazi (Wazazi) na mandhari ya mtaani iliyoibua ujumbe wa wizi na udokozi kama kikwazo cha maendeleo (Paka). Kielelezo Na. 14.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kukidhi matakwa ya swali.

6. Mandhari, ni sehemu au mahali ambapo kazi ya fasihi hutendeka, Kwa Mfano, Msituni, darasani au Kanisani. Kwa kutumia diwani mbili ambazo ni FUNGATE YA UHURU iliyoandikwa na Mohamed S. Khatibu pamoja na CHUNGU TAMU iliyoandikwa na Theobald A. Mvungi. Kwa kuanza na diwani ya CHUNGU TAMU Watunzi wa Mashairi ni Weledi wa kuteua Mandhari yenye uwezo wa kufikisha ujumbe kwa jamii husika kama ifuatavyo:

Mandhari ya Manzese yameibua ujumbe kuwa Wazazi hawapaswi kuyaingilia Mahusiano ya kimapenzi kati ya mtu na mtu, kwa mfano katika diwani hii msanii ametumia shairi la "Manzese Mpaka Ostabei" kuonesha namna ambavyo wazazi huyaingilia Mahusiano ya kimapenzi yaliyopo kwa Watoto wao. Msanii anasema kuwa:

"Wa manzese kwanini Wamtaka
Ati Mchumba
Mchumba asiye baraka
Wa manzese atakulisha taka"

61 Mandhari ya pangoni yamaibua ujumbe kuwa unyonyaji na unyanyasaji hukwamisha Maendeleo katika jamii, kwa Mfano katika diwani hii Msanii ametumia shairi la "Chatu na Kuku" kuonesha namna ambavyo tabaka tawala huwanyonya na kuwanyanyasa tabaka tawaliwa. Msanii anasema kuwa;


"pango likawa Mahakama,
Mashari akapangiwa
paku utaishi hapa na kulaga
Wanao watalunzwa
Na watatii amri"

pia katika jamii mbalimbali wapo watu kama hawa chatu wanaowapangia kuku Mashart.

Mandhari ya nyumbani (sebuleni) kwa Ana na Nania, yamefikisha ujumbe kuwa usaliti katika ndoa hukwamisha Maendeleo, kwa Mfano katika diwani hii Msanii ametumia shairi la "Fikra za wangu ana" kuonesha Mandhari ya nyumbani kwa Anna na Nania. Msanii anasema:

"Mume wangu nakupenda,
Joseph amenikuna,
Nimekula naye tunda,
Nimpendelea sana,
Ila usiyanze inda, Mimi ni wako kimwana
Nitaishi kwa Mpango, kwako na kwake Joseph

pia katika jamii mbalimbali wapo watu kama Anna



6. Pia kwa upande wa diwani ya FUNGATE YA UHURU watunzi wa mashairi ni weledi wa kuteua mandhari yenye uwezo wa kufikisha ujumbe kwa jamii kama ifuatavyo;-
Mandhari ya Hospitalini (thieta) yameibua ujumbe kuwa viongozi wasaliti hukwamisha maendeleo katika jamii, kwa mfano katika diwani hii msanii ametumia shairi la "Mjamzito" kuonesha namna ambavyo viongozi huwasaliti wananchi wao katika matatizo mbalimbali. Msanii anasema kuwa;
"Mjamzito amelazwa "Thieta"
Lazima kupasuliwa"
pia katika jamii mbalimbali wapo watu na viongozi ambao huwasaliti wananchi wao katika shida na matatizo.
Mandhari ya Msikitini, hekaluni, Kanisani na Ofisini yameibua ujumbe kuwa wizi ni kikwazo cha maendeleo katika jamii, kwa mfano katika diwani hii msanii ametumia shairi la "Wizi" kuonesha namna ambavyo watu huibiwa katika sehemu mbalimbali Msanii katika shairi hili anasema:
"Wizi umo,
Kanisani,
Msikitini,
Hekaluni."
Wanyang'anywao ni waumini"
Pia katika jamii mbalimbali wapo watu wanaoibiwa mali zao sehemu mbalimbali.

**Kielelezo Na. 14.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6

Kielelezo Na. 14.1 ni sampuli ya sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyetathmini kwa usahihi ukweli wa kauli kuwa “Watunzi wa mashairi ni weledi wa kuteua mandhari yenye uwezo wa kufikisha ujumbe kwa jamii

husika." Aidha, alibaini *mandhari ya hospitali* na kutoa mfano wa shairi la *Mjamzito* lenye ujumbe wa *viongozi* waoga badala ya wasaliti kama lilivyofafanuliwa. Pia, mtahiniwa aliandika utangulizi mzuri na hitimisho zuri linaloendana na swali, hivyo kupata alama za juu katika swali hili.

Aidha, asilimia 10.15 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuthibitisha ukweli wa kauli, "Watunzi wa mashairi ni weledi wa kuteua mandhari yenye uwezo wa kufikisha ujumbe kwa jamii husika*"* kwa kutoa baadhi ya hoja sahihi katika diwani moja na kushindwa katika diwani nyingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika diwani ya "Fungate ya Uhuru" alishindwa kubainisha ujumbe unaopatikana katika *mandhari ya kanisani* kutokana na uchaguzi usio sahihi wa shairi linalooonesha mandhari hiyo. Mtahiniwa mwingine alieleza kwa usahihi *mandhari ya kanisani* iliyoibua ujumbe wa watu kuachana na wizi na *mandhari ya msituni* iliyoibua ujumbe wa kujitoa mhanga. Hata hivyo, walitoa mifano ya mashairi yasiyo sahihi kwa mfano, shairi la *Golira* lilitokana na mandhari ya msituni lakini lilizungumziwa katika mandhari ya kanisani badala ya shairi la wizi, hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache asilimia 2.63 waliojibu swali hili, walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa umahiri kuhusu mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi*. Watahiniwa wengi katika kundi hili walimudu kutoa hoja moja hadi mbili zilizokuwa sahihi, lakini katika hoja nyingine walitoa maelezo yasiyojitosheleza. Pia, wengine walitoa mifano ya mashairi ambayo hayana mandhari walizozieleza katika hoja zao. Vilevile, watahiniwa hao walitumia mandhari ambazo zinatoa ujumbe usiolingana na maudhui katika shairi husika.

Kutokana na watahiniwa katika kundi hili kushindwa kuelewa matakwa ya swali hili ipasavyo, wapo waliojadili namna mandhari zilivyoibua dhamira mbalimbali. Kwa mfano, katika diwani ya "Kimbunga" walijadili dhamira kama vile; *rushwa, kufanya kazi kwa bidii,* na *kufanya mapinduzi*. Pia, katika diwani ya "Chungu Tamu" walijadili dhamira kama vile; *ubaguzi wa rangi* na *uzalendo* lakini hawakubainisha kwa usahihi mandhari zinazoibua ujumbe unaotokana na dhamira hizo. Kwa ujumla, watahiniwa

hao walishindwa kutathmini namna watunzi wa diwani teule walivyokuwa weledi wa kuteua mandhari yenye uwezo wa kufikisha ujumbe kwa jamii husika kama swali lilivyotakiwa, hivyo kupata alama za chini. Kielelezo Na. 14.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili kwa kushindwa kukidhi matakwa ya swali.

6. Mandhari: ni picha au taswira mbalimbali zinazoweza kutumiwa na wandishi kwa lengo la kuweza kufikisha ujumbe katika jamii husika. Kwa kutumia mashairi ya "KIMBUNGA" na "FUNGATE YA UHURU" wandishi wameweza kutumia taswira mbalimbali ili kuweza kufikisha ujumbe katika jamii. Kwa kuanza na shairi la "Kimbunga" lililoandikwa na mwandishi "Haji Gora" taswira zimeweza kuonesha kama ifuatavyo.

Kimbunga; hii ni taswira iliyoweza kutumiwa na mwandishi kwa kuonesha mapinduzi yanayoweza kutokea katika jamii kwa kuondoa uongozi au utawala wenye kudidimiza watu wenye hali ya chini ambapo mwandishi ameweza kuonesha taswira katika shairi la "Kimbunga" ~~kama ifuatavyo~~ katika ubeti

Kimbunga mji wa siyu, kilichowafikia si kwa yule wala huyu, ili kuwa patashika kiling'oa mibuyu na minazi kunusulika Nyayo zao zilitandaika

Hivyo, mwandishi ameweza kutumia taswira ya "Kimbunga" ili kuonesha mabadiliko juu ya jamii katika kuondo uongozi mbaya ili kujenga jamii mpya.

Chui; katika shairi hili mwandishi ameweza kutumia taswira ya chui

Kuweza kuonesha jinsi ukoloni mamboleo-
leo unavyoendelea kuathiri jamii mbali-
mbali ambapo mwandishi ameweza
kutumia taswira hii katika shairi
shairi la "Chui" ambapo anasema -
"Waliokuwa matajiri, kwao walipofika
Hawaweli kujisitiri, salama kujipatia
Waliokuwa mafakiri, kuzidi kuwaonea
Huyu ndiye chui gani?
Hivyo katika shairi hili mwandishi amew-
eza kuonesha jinsi ukoloni mamboleo
unavyozidi kuathiri jamii.
Kibwangai: mwandishi ameweza
kutumia taaswira hii kuweza kuelezea
jinsi watu wa tabaka la juu wanavyo-
tumia uongozi kwa kuathiri watu wa-
tabaka la chini ambapo mwandishi.
ameweza kutumia taswira hii katika
shairi la "Kibwangai" ambapo mwandishi
anasema -
"Kibwangai alijiona, ni mtu kakamilika
Akaanza kujivuna, na dharau kuzidia
Wala hata hakujali; wezake walimwambia
Akajiona hawi nyani umbo lile litadumu
Katika shairi hili mwandishi ameone-
sha namna watu wa hali ya juu
wanavyotumia madaraka yao vibaya
na kuathiri watu wa hali ya chini.
Kwa kumaliza na shairi la
"Fungate ya Uhuru" lililoandikwa
na mwandishi "Mohamed Khatibu"
ameweza kutumia taswira


**Kielelezo Na. 14.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika swali la 6

Kielelezo Na. 14.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeonesha namna taswira zilivyoibua dhamira mbalimbali katika diwani ya “Fungate ya Uhuru”. Pia, katika utangulizi alitoa maana ya mandhari isiyo sahihi na kutoa hitimisho lisiloendana na swali.

### 2.2.2.3 Swali la 7: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, mada ndogo ya *Uhakiki wa Riwaya*. Swali lilipima uwezo wa mtahiniwa wa kuchambua mitindo ya uandishi katika riwaya teule. Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja tatu kwa kila riwaya kuonesha jinsi mtindo wa riwaya hizo unavyofanana na unavyotofautiana.

Watahiniwa 23,146 sawa na asilimia 56.9 walijibu swali hili. Ufaulu wa swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 17,722 sawa na asilimia 76.57 walipata alama kuanzia 6.5 hadi 20. Chati Na.15 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kiasilimia katika swali la 7.




**Chati Na. 15**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Katika Chati Na. 15, watahiniwa 1,738 sawa na asilimia 7.51 walikuwa na ufaulu wa juu kuanzia alama 12 hadi 20, watahiniwa 15,984 sawa na asilimia 69.06 walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5, na watahiniwa 5,424 sawa na asilimia 23.43 walifaulu kwa kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa asilimia 7.51 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 12 hadi 20. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi* hususani mada ndogo ya *Uhakiki wa Riwaya*. Hata hivyo, watahiniwa wengi katika kundi hili walipata alama kuanzia 15 hadi 17 kutokana na majibu yao kuwa na mapungufu katika maelezo ya hoja zao kama vile; kutoa hoja tatu sahihi za mfanano na hoja mbili sahihi za kutofautiana na kushindwa

kutofautisha kwa usahihi hoja moja. Kwa ujumla, watahiniwa waliweza kufananisha na kutofautisha kwa usahihi mtindo waliotumia waandishi wa riwaya ya “Vuta N’kuvute”, “Usiku Utapokwisha” na “Mfadhili” kwa kuzingatia mtindo wa kila mwandishi. Baadhi ya hoja za mfanano wa mtindo walizotoa katika riwaya ya “Vuta N’kuvute” na “Mfadhili”, ni kuwa wote wametumia *mtindo wa barua*; *majibizano*, *masimulizi* na *mtindo wa nafsi*. Kwa upande wa kutofautiana kwa waandishi wa riwaya hizo walitoa hoja kama vile; *mtindo wa matumizi ya simu* kwenye “Mfadhili” lakini kwenye riwaya ya “Vuta N’kuvute” hakukuwa na matumizi ya simu. Kielelezo 15.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili kwa kukidhi matakwa ya swali.

7. Mtindo, ni upekee wa mwandishi katika uandishi wa kazi za fasihi. Waandishi wa kazi za fasihi huwa na namna ambayo huwatofautisha na waandishi wengine au kati ya mwandishi mmoja na mwingine. Mitindo ya waandishi huweza kufanana na pia kuweza kutofautiana. Kauli hii inathibitishwa katika riwaya ya MFADHILI iliyoandikwa na Hussein Tuwa pamoja na riwaya ya VUTA N'KUVUTE iliyoandikwa na Shafi Adam Shafi, waandishi hawa wanafanana na kutofautiana kimtindo katika riwaya zao.

~~K~~ Ufuatao ni ufanano wa mtindo kati ya riwaya ya Mfadhili na riwaya ya vuta n'kuvute.

Matumizi ya barua, waandishi wa riwaya hizi wote wametumia mtindo wa barua ili kukamilisha ujumbe uliokusudiwa kama inavyoonekana katika riwaya ya mfadhili mwandishi ameonesha matumizi ya barua pale ambapo Nyambuja alimwandikia Gaddibullah barua ya kumuaga, kama inavyo onekana Gaddibulla anasema "ananiandikia barua, kama mwanafunzi pia katika riwaya ya vuta n'kuvute barua imetumika pale ambapo Bwana Raza alimwandikia barua mjomba wake Yasmini baada ya Yasmin kutoroka. Hivyo mtindo huu umesaidia dhamira ya ujalidi.


Mtindo wa majibizano, pia katika riwaya hizi waandishi wametumia mtindo wa majibizano au dayalojia ambapo

7 tunaona katika riwaya ya Mfadhili kuna majibizano kati ya Dania na Nunu wakati Nunu alipokuwa akimshauri Dania baada ya kuachana na Gaddi bullah pia katika riwaya ya Yuta nkuvute kuna majibizano kati ya Yasmini na Mjomba wake baada ya Yasmini kumtoroka Bwana Raza. Mtindo huu unaibua dhamira ya Mapenzi ya dhati na uhalisia.

Mtindo wa nafsi, katika riwaya hizi kuna matumizi makubwa ya mtindo wa nafsi kwani waandishi wa riwaya wametumia nafsi zote tatu yaani nafsi ya kwanza nafsi ya pili na ya tatu kwenye umoja na wingi: Mfano katika riwaya ya Mfadhili mwandishi amatumia nafsi ya pili umoja kwa Gaddibullah alivyojitambulisha baada ya kuandikiwa barua na Miyambwa anasema "Ananiandikia barua kama mwanafunzi...!" pia katika riwaya ya Yuta nkuvute mwandishi amatumia mtindo wa nafsi ya kwanza wingi ona pale Denge na kundi lake wanapopambana na wakoloni. Hivyo huu ni ufanano wa mtindo ya waandishi.

Zipuatazo ni hoja zinazoonesha namna mtindo wa riwaya hizi unavyofanana.

Mtindo wa matumizi ya simu, waandishi wa riwaya hizi wamefanana katika mtindo huu, kwani mtindo wa simu amatumiwa katika riwaya ya mfadhili pekee pale ambapo Dania, Nunu na



7. Boazi walimwaliana kwa njia ya simu walipokuwa wakimtafuta Bi Hanuna lakini katika riwaya ya Vuta n'kuvute mtindo huu haujatumika kabisa. Hivyo mtindo huu unawatofautisha waandishi hawa.

Mtindo wa nyimbo, mtindo huu unawatofautisha pia waandishi wa riwaya hizi kwani kwa kiasi kikubwa umetumika katika riwaya ya Vuta N'kuvute pale ambapo Mwajuma alikuwa akimwimbia Yasmini nyimbo za majungu walipogombana. lakini katika riwaya ya Mfadhili mtindo huu haujatumika na mwandishi hivyo imepelekea kutofautiana.

Tofauti katika matumizi ya mtindo wa masimulizi, vilevile mtindo wa masimulizi umetofautiana katika riwaya hizi kwani mwandishi wa riwaya ya Vuta n'kuvute ametumia masimulizi kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na riwaya ya Mfadhili mfano katika riwaya ya Vuta N'kuvute masimulizi yametumika wakati Yasmin na Denge walipokuwa wakisimuliana kuhusu historia za maisha yao lakini pia Yasmin alipokuwa akimsimulia Mwajuma kuhusu maisha aliyoishi na Bwana Raza.

Hivyo, waandishi hutumia mitindo mbalimbali ili kufikisha dhamira na dhamira mbalimbali katika jamii husika mfano wa dhamira hizo ni kama vile Usaliti, Ulevi, Mapenzi, kujitoa muhanga na Umoja na mshikamano ili kuelimisha jamii juu ya mambo mbalimbali.

**Kielelezo Na. 15.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 7


Kielelezo Na. 15.1 ni sampuli ya sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeonesha kwa usahihi jinsi mtindo wa riwaya ya "Vuta N'kuvute na "Mfadhili" unavyofanana na unavyotofautiana na kutoa hoja tatu kwa kila riwaya kama swali lilivyomtaka.

Aidha, zaidi ya nusu ya watahiniwa waliojibu swali hili, asilimia 69.06 walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 6 hadi 14. Ufaulu huu ulitokana na baadhi yao kuonesha kwa usahihi baadhi ya mitindo ya riwaya teule inavyofanana na inavyotofautiana na kushindwa mingine. Watahiniwa wengine waliweza kuonesha kwa usahihi jinsi mtindo wa riwaya hizo unavyofanana kwa kutoa hoja tatu sahihi lakini walishindwa kuonesha tofauti sahihi za mitindo ya riwaya hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alionesha mtindo uliotumika katika riwaya ya "Vuta N'kuvute" kuwa ni; *matumizi ya barua iliyoandikwa na Shihabu kwenda kwa Yasmini*, *matumizi ya nyimbo* za *kuhamasisha watu kudai uhuru* na *matumizi ya nafsi*. Katika riwaya ya *"*Mfadhili" mtahiniwa huyo alionesha mtindo uliotumika kuwa ni; *matumizi ya barua ya Nyambuja aliyomwandikia Gaddi Bulla* na *mtindo wa masimulizi*. Hivyo mtahiniwa huyo alionesha mtindo wa riwaya unavyofanana katika *mbinu ya kimasimulizi*, *mbinu ya nafsi zote tatu* na *mbinu ya hadithi ndani ya hadithi*; lakini alitofautisha isivyo sahihi kama vile; *tofauti katika usimuliaji, majibizano* na *mtindo wa nyimbo*; tofauti ambazo si sahihi, hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, asilimia 23.43 ya watahiniwa waliofanya swali hili, walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa umahiri katika uhakiki wa mitindo ya riwaya teule. Baadhi, walijadili dhamira mbalimbali zilizotumiwa na waandishi wa riwaya teule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja kwa kutumia riwaya ya "Vuta N'kuvute" alibaini *mtindo wa lugha, mtindo wa moja kwa moja* na *mtindo wa pekee*; na katika riwaya ya "Mfadhili" alijadili *mtindo wa tamathali za semi* isivyo sahihi. Majibu hayo yalitokana na mtahiniwa huyo kushindwa kujua kuwa, mtindo ni upekee unaomtofautisha mwandishi mmoja na mwingine katika kazi ya fasihi.

Pia, watahiniwa wengine waliandika utangulizi usioendana na swali na wengine hawakuandika hitimisho. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika utangulizi alitoa maana ya *mtindo kuwa ni fani*, maana isiyo sahihi kwani *mtindo* ni jinsi mtunzi anavyotumia ufundi na hisia zake ili kuonesha upekee wa kazi yake; na *fani* ni umbo la nje la kazi ya fasihi au ufundi wa kisanaa anaotumia mtunzi katika kuumba kazi yake, hivyo mtindo ni moja ya kipengele kinachoshughulikiwa katika fani. Kielelezo Na. 15.2

kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili na kupata 0.


7. Kwa kutumia riwaya mbili ambazo ni Mfadhi
li iliyoandikwa na Hussein Tuwa pamoja na Riwaya ya
Vuta nikuvute iliyoandikwa na shafi Adam Shafi.
Mwandishi ameonesha namna mtindo wa riwaya hizo uli
vyofanana na kutofautiana, mtindo ni namna mwandishi
alivyotumia lugha na mpangilio wa matukio na visa katika ka
zi yake ya Sanaa. Zifuatazo ni tof kufanana kwa riwaya
hizo mbili
Suala la Matabaka, hapa waandishi wote wawili
wameongelea suala la matabaka lililojitokeza katika kazi zao
MFANO katika riwaya ya Kivuli kinaishi tunamuona Bi Kitle
mbe ambaye anaishi tabaka la juu kama kiongozi ambaye
anatumia uongozi wake kufanya anachoweza, pia katika kita
bu cha Nguzo mama tunamuona mwenyekiti anavyoweza ku
wa kiongozi asiye na [illegible] kwa kutokuwa na maadili kwa watu
wale wake, hii moja kwa moja inaashiria kufanana kwa waandi
shi hawa katika kazi zao.
Suala la Umasikini, umasikini ni ile hali ya mtu
kushindwa kujipatia mahitaji yake ya msingi, katika riwaya hii
tunaona ambavyo mwandishi amesimulia kuhusu umasikini
ulivyokuwa tatizo katika jamii MFANO katika jamii ya wat
u wa Bininingi wananchi wengi hali yao ya maisha ipo duni hali inay
opelekea kuishi kwa utawala wa [illegible] Kilembe ambaye anaonesha
dharau, pia katika riwaya ya Nguzo Mama tunaona namna
wananchi wa Patata wanasumbuliwa na Umasikini MFANO
Bi Saba ambaye ameolewa mjane na [illegible] kwa ajili ya [illegible]
wa na mumewe na hivyo kutokana umasikini, jamii inapaswa ku
jitambua kwa kujipatia kazi mwendi ye kufanya ili kuondoa umasikini
Suala la Uongozi mbaya, Hii ni ile hali ambayo
kiongozi anapewa nafasi ya kuongoza lakini anatumia vibaya ile
kazi au nafasi aliyopewa ambo katika riwaya hii ya Kivuli ki
naishi tunamuona namna Bi Kilembwe alivyokuwa kiongozi m
baya maana alikuwa dikteta katika uongozi wake MFANO bi Ki
lembwe alikuwa anataka awe ya kufanya jambo lolote atakalo,

**Kielelezo Na. 15.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Katika Swali la 7


Kielelezo Na. 15.2 kinaonesha sehemu ya sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejadili dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya ya “Kivuli Kinaishi” na “Nguzo Mama” japokuwa katika utangulizi wake alitaja

riwaya "Mfadhilli" na "Vuta N'kuvute" hali inayoonesha kuwa, mtahiniwa huyo alichanganya riwaya na tamthiliya kinyume na matakwa ya swali hili.

### 2.2.2.4 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, katika mada ndogo ya *Uhakiki wa Tamthiliya*. Swali lilimtaka mtahiniwa kupendekeza mbinu nne zilizotumiwa na waandishi katika kufikia ukombozi halisi kwa kutumia tamthiliya mbili alizosoma.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 34,356 sawa na asilimia 84.40 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Kati yao, watahiniwa 33,179 sawa na asilimia 96.57 walifaulu vizuri kwa kupata alama kuanzia 7 hadi 20. Chati Na.16 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 16**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Katika Chati Na. 16, watahiniwa 30,971 sawa na asilimia 90.14 walikuwa na ufaulu mzuri kuanzia alama 12 hadi 20, watahiniwa 2,208 sawa na asilimia 6.43 walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5, na watahiniwa 1,177 sawa na asilimia 3.43 walifaulu kwa kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5.

Takwimu za ufaulu zinaonesha kuwa, swali hili lilijibiwa vizuri sana na idadi kubwa ya watahiniwa ambapo asilimia 90.14 walikuwa na ufaulu

mzuri kuanzia alama 12 hadi 20. Miongoni mwao, watahiniwa 21,371 sawa na asilimia 62.12 walijibu vizuri zaidi na kupata alama za juu 16 hadi 20. Ufaulu huu mzuri ulitokana na watahiniwa kuwa na umahiri wa kutosha kuhusu mada ndogo ya *Uhakiki wa Tamthiliya*. Watahiniwa hao walipendekeza kwa usahihi mbinu nne kwa kila tamthiliya walizotumia waandishi katika kufikia ukombozi halisi katika tamthiliya mbili walizosoma. Mbinu sahihi zilizopendekezwa ni hizi: "Kwenye tamthiliya ya "Ukingo wa Thimu" walipendekeza jamii kuondokana na imani potofu, kupiga vita dhuluma, mila na desturi zilizopitwa na wakati na msimamo wa viongozi katika utekelezaji wa majukumu yao; katika "Nguzo Mama, zilipendekezwa mbinu kama kupiga vita uongozi mbaya, wanawake kupatiwa elimu, kupiga vita uzembe na uvivu, kusisitiza ushirikiano kati ya wanawake na wanaume ili kuleta haki na usawa na wanawake kushiriki katika kazi za kuleta maendeleo; katika "Morani", kupiga vita uhujumu uchumi, matabaka, rushwa, usaliti na unafiki pamoja na kusisitiza umoja na mshikamano; na katika tamthiliya ya "Kivuli Kinaishi" walipendekeza kwa usahihi hoja ya kujitoa mhanga, watu kupewa elimu ya kujitambua, kuwafundisha watoto ili wajue mema na mabaya, kupiga vita rushwa na kupiga vita uongozi wa kidikteta. Watahiniwa hao walitoa mifano sahihi kutoka katika riwaya husika ili kukidhi matakwa ya swali hili.

Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alipendekeza mbinu sahihi walizotumia waandishi wa tamthiliya teule ambapo "Kwenye Ukingo wa Thimu" alipendekeza; *kufanya kazi kwa bidii, kuwa jasiri, kupiga vita wivu wa kimaendeleo* na *wanawake kurithi mali za waume zao pindi wanapofariki*. Pia, katika tamthiliya ya "Nguzo Mama" alipendekeza *jamii kujiendeleza kielimu, kupiga vita usaliti, kupinga uongozi usifaa* na *kuepuka uvivu*. Pia, aliandika utangulizi mzuri na hitimisho zuri lililoendana na swali, hivyo kupata alama za juu. Kielelezo Na. 16.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili.

08· Suala la ukombozi ndio kilio kikuu
cha waandishi wengi katika karne ya ishirini
ni na moja. Ukombozi ni kitendo cha mtu -
kuwa na uelewa wa kufanya mambo mazuri -
na kuyaacha mambo yote mabaya na yanayo-
kwamisha maendeleo katika jamii. ~~Kwa~~ Kutu-
mia Tamthiliya ya "Kwenye Ukingo wa -
Thim" mwandishi ni Ebrahim Hussein -
na kutumia tamthiliya ya "Nguzo Mama"
mwandishi ni Penina Muhando. Waandishi
hawa wameweza kutoa mbinu zitakazotumi-
wa na watu katika kufikia ukombozi -
halisi.
Kwa kuanza kutumia tamthiliya-
ya KWENYE UKINGO WA THIM msanii amewe-
za kuonesha mbinu za kufikia ukombozi -
halisi kama ifuatavyo; -
Kufanya kazi kwa bidii, hiki ni -
kitendo cha mtu kuwa na uelewa wa ku-
fanya jambo au kazi kwa lengo la kuji -
komboa katika umaskini. Kwa mfano -
mhusika "Martha" anaoneshwa akipata -
nishani ya ufanyakazi bora, ~~hivyo~~ kama
ifuatavyo; -
"Pasta; Unakumbuka ulipopata nishani
ya ufanya kazi bora, unakumbuka
mwanamke - - - - - - ".
Hapa inadhihirisha kitendo cha Martha -
kujikomboa katika umaskini.
Kuwa jasiri, katika tamthiliya hii
mwandishi anaweza kuonesha kuwa -
jamii imepata ukombozi wake. Kwa -

08. mfano katika tamthiliya hii kuna mhusika aitwaye "Martha", mhusika huyu anaonesha akipigana vita vya Maumau huko nchini Kenya. Hivyobasi kitendo hiki kinaweza kuwa kama mbinu katika kufikia ukombozi halisi katika jamii.

Kupiga vita wivu wa kimaendeleo, huu ni wivu unaoonekana katika tamthiliya hii na ambao unakwamisha maendeleo katika jamii. Mfano kutoka katika tamthiliya hii ya "Kwenye Ukingo wa Thim" msanii anasema;-

"Pasta; Unakumbuka ulipopata nishani ya ufanyakazi bora, Unakumbuka, mwanamke!, ulijiona wewe ndio wewe".

Hivyobasi hii ni mbinu inayothibitisha hatua ya kufikia ukombozi halisi katika jamii zetu tunazoishi.

Wanawake warithi mali za waume zao pindi ~~wanapo~~ waume zao wanapofariki, katika tamthiliya hii inaonesha desturi ya wanawake kutokurithi mali za waume zao, kitendo ambacho kinaweza kukwamisha malengo ya kufikia ukombozi halisi. kwa mfano katika tamthiliya hii ni

"Martha; Baba yako kafariki, katuachia kichwa cha tembo lakini meno na usinga kawapa Umma Klan"

Hivyobasi wanawake wakiruhusiwa kurithi mali za waume zao baada tu ya waume zao kufariki itakuwa tumefikia ukombozi halisi

08· Vilevile kwa kutumia kitabu cha tamthiliya ya NGUZO MAMA msanii-amewezq kuonesha mbinu mbalimbali za kufikia ukombozi halisi katika jamii zetu kama ifuatavyo ;-

Jamii ijiendeleze kielimu, hii ni mbinu mojawapo ya jamii kuwa na-ukombozi halisi katika kujiendeleza-kimaendeleo. Kwa mfano kutoka katika-tamthiliya hii ya "Nguzo Mama, msanii-anasema

"Bi Nane, tutumie kamba kuinua Nguzo Mama"

Huu ni ukombozi wa kielimu ambao anao Bi Nane tu, hivyo hii ni mbinu halisi ya kufikia ukombozi katika jamii.

Kupiga vita usaliti, hiki ni kitendo-cha kukiuka makubaliano baina ya watu. Kwa mfano Bi Tatu anamsaliti Chizi kama mwandishi anavyosema;-

"Chizi; Shangazi nina njaa,
Bi Tatu; Toka hapa,
Chizi; Shangazi sina nguo,
Bi Tatu; Toka hapa, usiniite shangazi, ukiendelea tena nitakuitia mbwa akuume".

Pia kitendo hiki cha kupiga vita usaliti ni nyenzo ya kufikia ukombozi halisi katika jamii zetu.

Kupiga vita uongozi mbaya, huu ni uongozi ambao unakandamizo watu katika jamii, kitendo ambacho kinamfanya mtu kutokuwa huru na kushi-

08. ndusa kupata nafasi ya kujieleza -
katika uongozi huo. Kwa mfano katika
tamthiliya hii, kuna uongozi mbaya wa
mwenyekiti ambapo, kiongozi huyu -
anabagua watu wa kuwasikiliza katika
kupeleka malalamiko yao mbele ya haki.
Mfano Bi Nne anamshitaki Bi Nane -
jambo ambalo si la haki. Bi Nane -
anasema

"Bi Nane; Kama nashtakiwa, nieleze ni kwa
kosa gani"

Hivyobasi kitendo hiki kinaweza kutufanya -
tukafikia ukombozi halisia.

Kupiga vita uvivu, hii ni hali ya
mtu kuwa katika tabia ya kujiendekeza
kutokufanya kazi katika jamii zetu.
Kwa mfano, kuna mhusika aitwaye Bi
Moja, ni mhusika ambaye ni mvivu kama
msanii anavyosema; -

Bi Moja; Ndani aji kalia, miguu kuji-
nyoosha na domo kujipigia

Pia hii inadhihirisha kuwa tutafikia -
ukombozi halisi endapo tutapiga vita
uvivu.

Hivyobasi, kutokana na mbinu anazo-
zitumia mwandishi katika kufikia uko-
mbozi halisi, kuna taarifa au jumbe-
mbalimbali ambazo wanajamii wana-
zipata kama vile kujiendeleza kieli-
mu, kupiga vita mapenzi yasiyo ya -
dhati pamoja na kupiga vita usaliti -
katika jamii zetu.

**Kielelezo Na. 16.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 8

Kielelezo Na. 16.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyependekeza kwa usahihi mbinu nne walizotumia waandishi wa tamthiliya za "Kwenye Ukingo wa Thimu" na "Nguzo Mama" katika kufikia ukombozi halisi. Pia, aliandika utangulizi mzuri na hitimisho zuri lililoendana na swali na kupata alama zote 20.

Kwa upande mwingine, asilimia 6.43 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa wa kundi hili kupendekeza baadhi ya mbinu sahihi zilizotumiwa na waandishi katika kufikia ukombozi halisi na kushindwa mbinu nyingine. Aidha, watahiniwa wengine walitoa hoja sahihi lakini walitoa mifano isiyojitosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja kwa kutumia tamthiliya za "Nguzo Mama" na "Morani" alionesha kuwa jamii inahitaji *ukombozi kijamii, ukombozi wa kisiasa, ukombozi wa kiuchumi* na *ukombozi wa kiutamaduni*. Hata hivyo, mtahiniwa alishindwa kupendekeza mbinu anuwai zilizotumiwa na waandishi katika nyanja hizo ili kufikia ukombozi halisi, hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache sawa na asilimia 3.43 walijibu vibaya swali hili na kuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa umahiri wa mada ndogo ya *Uhakiki wa Tamthiliya*. Baadhi ya watahiniwa walijadili vipengele vya fani na maudhui katika tamthiliya teule. Kwa mfano mtahiniwa mmoja kwa kutumia tamthiliya za "Morani" na "Kivuli Kinaishi" alibaini vipengele vya fani kama vile *muundo, mtindo, wahusika* na matumizi ya lugha. Kwa upande wa maudhui alijadili dhamira, ujumbe na falsafa. Hii inaonesha kuwa mtahiniwa huyo hakuwa na uelewa juu ya mbinu zilizotumiwa na waandishi katika kufikia ukombozi halisi. Aidha, mtahiniwa huyo aliandika utangulizi uliokidhi matakwa ya swali kiasi cha kupata alama 1. Kielelezo Na. 16.2 kinaonesha sampuli ya sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili kwa kushindwa kukidhi matakwa ya swali na kupata alama za chini.

8. Ukombozi ni hali ya mtu au jamii kujikomboa katika nyanja mbalimbali zikiwemo za kiutamaduni, kisiasa, kifikra na ukombozi. Ni kweli kabisa kuwa suala la ukombozi ndio kilio kikubwa cha waandishi katika karne ya ishirini na moja. Kauli hii inaweza kuthibitishwa kwa kutumia tamthiliya mbili ambazo ni, NGUZO MAMA yake penina Mhando na KIVULI KINAISHI yake Said mohamed.

Kwa kuanza na thamthiliya ya NGUZO MAMA yake, penina mhando, mwandishi amependekeza mbinu zifuatazo;

Matumizi ya lugha ya kishairi ili kuonyesha ukombozi, mwandishi ametumia lugha yenye ushairi ndani yake ili kuhimiza jamii kuwa tunapaswa kuungana kama inavyosema;

"Tufanye maandamano
maazimio tuyatoe
Na sanaa tuipambe


mwandishi anaonyesha ni kwa jinsi gani wanawake wanapaswa kujikomboa kwa kushirikiana.

Matumizi ya nyimbo, mwandishi ametumia nyimbo ili kuonyesha ni kwa jinsi gani kwenye suala la ukombozi mwanamke anajikomboa mfano;

Nguzo mama, Nguzo mama
8 Tukupambeje mama?

nyimbo hii inatia hamasa kubwa kwa wanawake.

Matumizi ya nafsi, pia mwandishi ameweza kutumia nafsi ili kuonyesha ushirikiano



8' na kuhakikisha jamii ingaone kama inavyosema,
"— — — Nafikiri wote tunajua"
mwandishi ametumia nafsi ya III wingi kuonye-
sha ushirikiano.
'Matumizi ya mkarara, pia mwandishi ametumia
mbinu hii kuonyesha kuwa mwanamke anapaswa
kujikomboa kwanza na anamaanisha kuwa
ukombozi wa mwanamke ni yeye kwanza.
" Neno nguzo mama tukupambeje mara
limejitokeza mara nyingi.
"-- Nguzo mama tukupambeje mara?"
kupitia mbinu mwandishi anaihasa jamii
kuwa ili mtu kujikomboa ni yeye tu
na maamuzi yake.
pia kwenye tamthiliya ya MORANI yake
Emmanuel mbogo, mbinu zifuatazo zimetolewa
na mwandishi,
Matumizi ya Matangazo, mwandishi ametumia
mbinu ya matangazo kuonyesha kuwa jamii
inapaswa kuwa na umoja na ushirikiano
ili kutatua matatizo,
ZAMBAMBO! LA MBAMBO!
WANANCHI!
WAFANYAKAZI!
WAKULIMA!
MNATANGAZIWA KUWA KESHO KUTAKUWEPO NA
MAANDAMANO YATAKAYOANZIA MAKAO MAKUU
8' YA MORANI ILI KUPINGA UBEPARI,
UHUJUMU UCHUMI, RUSHWA
VIJANA OYEEE!!
matumizi ya majigambo yanaonyesha kuwa
jamii inapaswa kuwa na ushirikiano.

**Kielelezo Na. 16.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 8

Kielelezo Na. 16.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili kwa kujadili mitindo waliyotumia waandishi katika kazi zao badala ya kupendekeza mbinu nne zilizotumiwa na waandishi kufikia ukombozi halisi.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa somo la Kiswahili unaonesha kuwa mada 12 zilitahiniwa ambapo mada nane (8) zilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Mada hizo ni *Maendeleo ya Kiswahili* (98.99%), *Ufahamu na Ufupisho* (98.31%), *Tamthiliya* (96.57%), *Ushairi* (94.95%), *Utungaji* (94.54%), *Usanifu wa Maandishi* (92.51%), *Riwaya* (76.57%) na *Matumizi ya Sarufi* (71.08%). Aidha, mada nne (4) zilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu ambazo ni *Maendeleo ya Fasihi Simulizi* (51.68%), *Tafsiri na Ukalimani* (50.31%), *Fasihi kwa Ujumla* (47.60%) na *Utumizi wa Lugha* (37.85%). Licha ya ufaulu mzuri na wa wastani wa watahiniwa katika mada hizo, mada ya *Utumizi wa Lugha* ilikuwa na ufaulu wa chini zaidi ikilinganishwa na mada zote zilizotahiniwa katika mtihani huu.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2025 umepungua katika mada tisa (9) ikilinganishwa na mwaka 2024. Mada zilizopungua kiwango cha ufaulu ni *Ufahamu na Ufupisho* (98.31%), *Ushairi* (94.95%), *Utungaji* (94.54%), *Riwaya* (76.57%), *Matumizi ya Sarufi* (71.08%), *Maendeleo ya Fasihi Simulizi* (51.68%), *Tafsiri na Ukalimani* (50.31%), *Fasihi kwa Ujumla* (47.60%) na *Utumizi wa Lugha* (37.85%). Upungufu wa ufaulu kwa mada hizo ni asilimia 0.51, 1.73, 4.97, 23.02, 29.62, 6.84, 14.25 na 55.49 mtawalia. Hata hivyo, kuna mada chache ziliongezeka ufaulu ambazo ni: *Maendeleo ya Kiswahili* (98. 99%), *Tamthiliya* (96.57%), na *Usanifu wa Maandishi* (92.51%) kwa ongezeko la asilimia 6.7, 8.64 na 31.9 mtawalia.

Kiwango cha kushuka kwa ufaulu mwaka 2025 ikilinganishwa na mwaka 2024 kilitofautiana kati ya mada moja na nyingine ambapo mada ya *Utumizi wa Lugha* ilishuka kwa kiwango kikubwa cha asilimia 55.49 ikifuatiwa na mada za *Maendeleo ya Fasihi Simulizi*, *Riwaya* na *Fasihi kwa Ujumla* zilizoshuka kwa asilimia 29.62, 23.02 na 14.25 mtawalia. Hata hivyo, mada nyingine tano (5) zilizoshuka zilikuwa na mwachano mdogo wa ufaulu. Upungufu mkubwa wa ufaulu kwa baadhi ya mada unaonesha dhahiri kuwa, baadhi ya watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha wa mada hizo na wengine hawakuelewa matakwa ya baadhi ya maswali ipasavyo.

Licha ya mada ya *Utumizi wa Lugha* kuwa na matokeo ya chini zaidi (37.85%) kwa mwaka 2025, wastani wa ufaulu kwa mada zote ulikuwa mzuri ambapo, asilimia 75.92 ya watahiniwa wapata alama zaidi ya 35 katika mada zote. Hii inadhihirisha kuwa, watahiniwa walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu mada nyingi zilizotahiniwa ukihusisha uelewa wa dhana za kifasihi na kisarufi, matumizi sahihi ya lugha, umahiri wa lugha ya kiingereza, uzingatiaji wa alama za uandishi, uhakiki wa kazi za kifasihi,

ufahamu na ufupisho, usanifu wa maandishi ya kifasihi na utoaji wa hoja sahihi zenye mifano thabiti.

## 4.0 HITIMISHO

Taarifa hii inaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika mtihani wa 121 Kiswahili kwa mwaka 2025 kilikuwa kizuri kwani asilimia 99.98 ya watahiniwa waliofanya mtihani walifaulu. Ufaulu katika mada zote (12) ulikuwa mzuri ambapo wastani wa ufaulu ulikuwa ni asilimia 75.92. Ufaulu mzuri umetokana na watahiniwa kuwa na maarifa, ujuzi na weledi wa mada mbalimbali zilizotahiniwa. Kiwango hiki cha ufaulu wa watahiniwa ni cha chini kidogo kwa asilimia 0.02 kikilinganishwa na kiwango cha ufaulu wa mada cha mwaka 2024 ambapo wastani wa ufaulu wa mada zote ulikuwa asilimia 100.

Uchambuzi huu umebaini changamoto mbalimbali zilizosababisha ufaulu wa wastani katika mada za *Utumizi wa Lugha, Fasihi kwa Ujumla, Tafsiri na Ukalimani* na *Maendeleo ya Fasihi Simulizi.* Sababu hizo zinahusisha kutozingatiwa kwa maelekezo ya maswali ipasavyo na uelewa mdogo wa baadhi ya mada zilizotahiniwa. Ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa mada zote katika mitihani ijayo, mikakati mbalimbali inahitajika katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ambapo watahiniwa watapata umahiri na ujuzi wa kutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa ufasaha. Hatua hii ni muhimu hasa ikizingatiwa kuwa mtihani wa Kidato cha Sita unalenga kuandaa wataalam wa lugha ya Kiswahili kitaifa na kimaitafa.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ufaulu wa somo la Kiswahili ni mzuri kutokana na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali na wadau wengine wa elimu. Kwa ujumla, ili somo hili liendelee kuwa na ufaulu mzuri zaidi, yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu watumie mbinu shirikishi kama vile midahalo, mijadala, na makongamano katika ufundishaji na ujifunzaji ili kuwaongezea wanafunzi ujuzi na maarifa zaidi.

(b) Walimu wawaongoze wanafunzi kufanya ziara za kimasomo katika maeneo mbalimbali ili kujifunza kwa vitendo zaidi na kuwa mahiri katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

(c) Walimu waendelee kuwahimiza wanafunzi kuongeza juhudi katika kutumia lugha sanifu ya Kiswahili kwa ufasaha.

(d) Walimu wawahimize wanafunzi kusoma vitabu vya kiada na ziada na majarida/machapisho mbalimbali yanayohusiana na kanuni na matumizi ya lugha sanifu ili wawe na uelewa wa kutosha.

(e) Walimu watumie njia ya majadiliano, maswali na majibu, bungua bongo, na vielelezo wakati wa ufundishaji na ujifunzaji ili wanafunzi wajifunze kwa vitendo na wawe mahiri zaidi.

***Kiambatisho A* : UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MWAKA 2025**

**121 Kiswahili**

| **Na.** | **Mada** | **Idadi ya Maswali** | **Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa kwa Mada** | **Maoni** |
|---|---|---|---|---|
| *1.* | *Maendeleo ya Kiswahili* | 2 | 98.99 | Vizuri |
| *2.* | Ufahamu na Ufupisho | 1 | 98.31 | Vizuri |
| *3.* | *Tamthiliya* | 1 | 96.57 | Vizuri |
| *4.* | *Ushairi* | 2 | 94.95 | Vizuri |
| *5.* | *Utungaji* | 1 | 94.54 | Vizuri |
| *6.* | *Usanifu wa Maandishi* | 1 | 92.51 | Vizuri |
| *7.* | *Riwaya* | 1 | 76.57 | Vizuri |
| *8.* | *Matumizi ya Sarufi* | 2 | 71.08 | Vizuri |
| 9. | *Maendeleo ya Fasihi Simulizi* | 2 | 51.68 | Wastani |
| 10. | *Tafsiri na Ukalimani* | 1 | 50.31 | Wastani |
| 11. | *Fasihi kwa Ujumla* | 1 | 47.60 | Wastani |
| 12. | *Utumizi wa Lugha* | 1 | 37.85 | Wastani |

***Kiambatisho B :*** **ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MWAKA 2024 NA 2025**

